**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 16 Novemba, 2007**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma* Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)**:-

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2006.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2004/2005 *(The Annual Report and Accounts of the Road Fund Board for the Year 2004/2005)* .

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 187

**Mahitaji ya Hospitali ya Wilaya – Kigoma Vijijini**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, pamoja na juhudi mbalimbali za Serikali za kuboresha huduma za afya nchini, bado tatizo ni kubwa katika Mkoa wa Kigoma kutokana na kukosekana kwa hospitali ya Wilaya, hali inayosababisha hospitali ya Mkoa kuelemewa na wagonjwa wengi hivyo kushindwa kuwamudu na kusababisha vifo visivyo vya lazima vya watoto na akinamama wajawazito wanaohitaji upasuaji baada ya kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida.

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kujenga hospitali ya Wilaya ya Kigoma Vijijini ili kuondoa matatizo yanayoikabili hospitali ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali halisi ya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na wakazi wa Wilaya ya Kigoma. Halmashauri ina jumla ya wakazi wapatao 598,139 kulingana na sensa ya mwaka 2002.

Kwa kuzingatia Sera ya Afya na kulingana na mkakati wa Taifa wa kujenga Zahanati kwa kila kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata, Wilaya ya Kigoma inapaswa kuwa na Hospitali moja ya Wilaya, Vituo vya Afya 17 na Zahanati 75.

Kwa sasa Wilaya hiyo ina Vituo vya Afya 5, vinne ni vya Serikali na kimoja ni cha Shirika la Dini, pia ina Zahanati 65 zikiwemo 59 za Serikali, na mbili za Mashirika ya dini na mbili za Mashirika Binafsi. Wilaya ya Kigoma haina hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona tatizo hili, imeanzisha mikakati wa makusudi ya kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa Wilaya ya Kigoma Vijijini. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuweka mkazo ujenzi wa Zahanati kwa kila kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata. Halmashauri pia imeweka mikakati ya kuboresha huduma zinazotolewa katika Vituo vya Afya ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Aidha, mikakati hiyo ni pamoja na kuviwezesha vituo vya Nguruka na Mgambo kutoa huduma ya kuongeza damu na kufanya upasuaji. Hivi sasa majengo ya vyumba hivyo vya upasuaji yako katika hatua za mwisho za ujenzi, na inategemewa kwamba ifikapo Februari, 2008 ujenzi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuendelea kuboresha huduma za afya Halmashauri imeweka mkakati wa kujenga hospitali ya Wilaya ya Kigoma. Hatua za awali za kujadili na kupitisha uamuzi huu katika vikao vya Halmashauri zimekwikufanyika na kwa kuzingatia makubaliano ya vikao vyote, eneo la Kata ya Kandaga, kijiji cha Kalange limekubalika litumike kwa ujenzi wa hospitali hiyo. Kwa sasa Halmashauri inaendelea kufanya mawasiliano na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili waweze kupata kibali cha kujenga hospitali hiyo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba maboresho mbalimbali yanafanyika katika Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo.

Lakini atakubaliana na mimi kwamba Zahanati nyingi hazina wauguzi, manesi wala hazina madawa. Je, ana mkakati gani tofauti na huo aliosema yeye?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba watumishi wengi wanakwenda katika Zahanati na Vituo vya Afya mbalimbali. Kwa mfano, katika Kituo cha Afya cha Nguruka kuna watumishi 25 kati ya watumishi 29. Kituo cha Afya cha Mgambo kuna watumishi 19 kati ya watumishi 29. Tatizo la upungufu wa watumishi ni kwa Tanzania nzima na Serikali imeweka mkakati wa kuwasomesha Madaktari wengi na Manesi wengi ili baadaye waweze kukidhi mahitaji ya Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona kwa kutaja Nguruka umemchokoza Mbunge wa Kigoma Kusini. Mheshimiwa Manju Msambya uliza swali la nyongeza.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vikao mbalimbali vimekwisha kukaa na kuamua kwamba Kijiji cha Kalenga katika Kata ya Kandaga ndipo patajengwa hospitali.

Lakini vilevile Mkoani kule kuna uamuzi wa vikao ambavyo vimekaa na vikasema kwamba watarithi majengo ya sehemu ya Lungufu ambako kuna Kambi ya Wakimbizi na ambapo majengo yanakidhi haja ili iwe hospitali ya Wilaya pale. Sasa uamuzi ni upi ni Kalenga au ni Lungufu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Spika, kulingana na vikao ambavyo vimekwishafanyika na vimepitisha kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata hadi Halmashauri ni kwamba Kalenga ndipo palipochaguliwa kujengwa hospitali ya Wilaya, kwa sababu ndilo eneo ambalo wameona kwamba ni muafaka kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Kama kutakuwa na maamuzi mengine basi ni kazi ya Halmashauri yenyewe kuamua ni vipi wafanye.

Lakini mpaka sasa hivi Vikao vya Halmashauri vimeamua kwamba Kalenga ndipo mahali muafaka kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo ya Wilaya. *(Makofi)*

Na. 188

**Tatizo la Ucheleweshaji wa Kesi**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI** aliuliza:-

Kwa kuwa, siku za hivi karibuni mahubusu kwenye baadhi ya Magereza walipotembelewa na baadhi ya Viongozi waliilalamikia Serikali kuwa, haifanyi kazi yake ipasavyo kwa kitendo cha mashauri yao kuchukua muda mrefu:-

(a) Je, nini chanzo cha ucheleweshaji wa kesi hizo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ukomo wa muda wa upelelezi na uchunguzi wa makosa ya jinai yaliyoainishwa katikA Kanuni ya Adhabu (*Penal Code*) Sura ya 16 ya Sheria za nchi unaratibiwa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na.9/1985.

Aidha, makosa mengine yote yaliyoainishwa na Sheria nyingine yanapaswa kuchunguzwa na kupelelezwa kwa mujibu wa Sheria zinazoainisha makosa husika. Utaratibu na ukomo wa muda wa uchunguzi kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai Na. 9/1985 umeelezwa katika kifungu cha 225 kuwa ni siku 60 isipokuwa kwa makosa yanayohusu uhaini, kughushi, kula njama za kughushi, mauaji, uhujumu uchumi na kadhalika isipokuwa pale ambapo kwa sababu maalum,

Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa, Wakili wa Serikali atakuwa amewasilisha hati ya kuomba kuongezewa muda (*Certificate of Adjournment*).

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika,sababu zinazochangia ucheleweshaji wa kesi ni mtambuka kwani zinahusu Wizara mbalimbali, Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi, Washitakiwa na mashahidi. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na:-

Upelelezi wa kesi hizo huchukua muda mrefu kwa sababu ya uhaba wa vifaa vya kisasa vya maabara kwa ajili ya kuchunguza vielelezo vya makosa ya Jinai *(Forensic Laboratory).*

Uwezo mdogo wa kitaalam na idadi ndogo ya Askari wa Idara ya Upelelezi.

Kuchelewa kupatikana kwa taarifa za uchunguzi wa vielelezo ikiwemo taarifa za vifo (*Post Mortem Report*) kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na hospitali husika.

Idadi ndogo ya Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali na wa Kujitegemea, hivyo kusababisha mlundikano wa kesi zinazosubiri kusikilizwa.

Mashahidi kukataa au kusita kufika Mahakamani kutoa ushahidi. Kukosekana kwa fedha za kuwalipa mashahidi ili waweze kufika Mahakamani kutoa ushahidi.

Baadhi ya mashahidi kuhama sehemu walizokuwa wanaishi hivyo kuchukua muda mrefu kuwapata ili kufika Mahakamani kutoa ushahidi.

Baadhi ya watuhumiwa kutokuwa wakweli wakati wa kutoa maelezo ya makosa wanayotuhumiwa nayo hivyo kufanya Askari kuchukua muda mrefu kutafuta ushahidi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Usalama wa Raia, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine wameweka mikakati mbalimbali ya kuharakisha usikilizaji wa kesi ikiwemo:

Kuimarisha Idara ya Upelelezi kwa kuongeza idadi ya Askari na kuwapa mafunzo ya upelelezi ndani na nje ya nchi;

Kuongeza vitendea kazi katika Idara za Upelelezi ikiwemo kuwapatia usafiri wa magari na pikipiki;

Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya wametakiwa kuzisimamia kwa karibu kesi zote zilizoko katika maeneo yao;

Jeshi la Polisi limeunda Tume ambayo itatembelea Mikoa yote kukagua majalada yote hasa yale ya kesi za muda mrefu, kuyasoma na kuyatolea maamuzi;

Kuendesha na kuharakisha vikao vya kusukuma kesi (*Case Flow Management Committee*) katika ngazi za Wilaya, Mikoa hadi Kanda na kupitia kesi zote za jinai na kuona sababu za ucheleweshaji wa kesi hizo na kuzitolea maamuzi;

Waziri wa Usalama wa Raia ameunda Kamati Maalum ndani ya Jeshi la Polisi ambayo jukumu lake ni kushughulikia malalamiko yote ya mahabusu na kuyapatia ufumbuzi kwa kushirikiana na Makamanda na Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa yote hapa nchini. Kamati hiyo imeanza kazi yake kwa kuanzia na Kanda Maalum ya Dar es Salaam;

Serikali pia inakusudia kujenga Chuo cha Upelelezi cha Polisi Mkoani Dodoma. Chuo hiki kitakapokamilika kitaweza kutoa wapelelezi wenye utaalam wa kupeleleza mashtaka yote kwa njia na mbinu za kisasa zaidi;

Jeshi la Polisi pia, limekamilisha ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi ya (*Forensic Bureau*) ambapo kwa kiasi kikubwa itaharakisha uchunguzi wa vidhibiti ambayo vitahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara;

Serikali iko katika hatua za mwisho za kutenganisha jukumu la kuendesha Mashtaka kutoka vyombo vya uchunguzi likiwemo Jeshi la Polisi ili iweze kubaki na jukumu la upelelezi kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi katika upelelezi.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Uraia. Nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza na kwa sababu ameishaonyesha mkakati ambao utachukuliwa hivi karibuni ili kuondoa tatizo la mlundikano wa mahabusu kwenye Magerezani yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa tatizo kubwa ambalo linaonekana ni ucheleweshaji wa kesi wa kuwachukua watuhumiwa mbalimbali kutoka Magerezani hasa Magereza ya Wilayani kuwapeleka Mahakamani. Tatizo hili linatokana na ukosefu wa askari wa kwenda kuwafuata mahabusu kwa wakati muafaka. Lakini pili kukosa vyombo vya usafiri vya kuwachukua mahabusu kwenda Mahakamani.

Je, Serikali sasa haioni jukumu hili la kuwapeleka hao wahalifu au watuhumiwa Mahakamani sasa waachiwe Askari Magereza kwa kuwapa vyombo maalum kusudi kuweza kuondoa mlundikano wa mahabusu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imekwishafanya uamuzi kwa Idara ya Magereza kuwa wao ndiyo watakaowapeleka na kuwarudisha wafungwa Mahakamani. Hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina mkakati wa kununua mabasi mapya kwa ajili ya kazi hiyo, na kwa kuanzia ina mkakati wa kununua mabasi ya *coaster* yenye kuchukua abiria 26 mpaka 32 mawili, kununua mabasi madogo yenye kuchukua abiria 26 mawili kwa kuanzia kwa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa, wapo mahabusu wanaokaa magerezani kwa miaka mingi bila kesi zao kutajwa kabisa Mahakamani na hilo huwa linatokana na nini? Hilo nina ushahidi nalo.

Kuna mtuhumiwa ambaye nilishawahi kumfuatilia mimi mwenyewe alikaa gerezani kwa miaka 10 bila kesi yake kutajwa Mahakamani mpaka mimi nilipofuatilia ndipo *file* lake likatafutwa na lilipatikana kwa muda wa mwezi mzima. Je, hiyo inatokana na nini?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza sababu nyingi sana katika jibu langu la msingi zinazosababisha kuchelewa kwa kesi na mahabusu kukaa kwa muda mrefu magerezani. Lakini kama nilivyosema kwamba sasa hatua zinachukuliwa kuhakikisha kwamba tatizo hilo linaondoka kabisa na ili wananchi wasipate usumbufu. *(Makofi)*

Na. 189

**Kuimarisha Kituo cha Polisi Itigi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, matukio ya ujambazi ya kutumia silaha yameongezeka kati ya Itigi na Tabora; na kwa kuwa, hali hiyo inatishia pia usalama wa abiria wanaosafiri kati ya Itigi –Chunya-Mbeya ambako kuna mapori makubwa:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupanua na kukiimarisha kituo cha Polisi cha Mjini Itigi kwa kuongeza idadi ya Askari na kukipatia gari na pikipiki kituo hicho kwa ajili ya doria na ulinzi wa raia na mali zao kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Itigi kimo katika mpango wa kupanuliwa na kuimarishwa ili kiweze kukidhi kasi ya ukuaji wa mji huo. Hata hivyo, utekelezaji wa nia hiyo ya Serikali utategemea uwezo wa Bajeti yake. Aidha, Serikali imepeleka Askari wapya 85 katika Mkoa wa Singida ambapo baadhi yao watapelekwa Itigi kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa Kituo cha Polisi Itigi kupatiwa gari. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Kituo cha Polisi cha Itigi kimepatiwa pikipiki moja mpya namba PT.1228 ili kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. Kwa sasa Kituo cha Polisi Itigi kitaendelea kupata huduma ya gari toka Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Manyoni. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha Doria, operesheni, misako ya mara kwa mara na kuwashirikisha wananchi katika masuala ya ulinzi (Polisi Jamii) ili kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Raia kwa wananchi wa maeneo hayo pamoja na wasafiri wanaotumia barabara ya Itigi-Tabora na Itigi Chunya.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inatambua ukubwa wa Jimbo langu na ukubwa wa Wilaya ya Manyoni kwa ujumla; na kwa kuwa, Kituo cha Mgadu ni Kituo ambacho kiko mbali sana kuja Itigi na kufika Makao Makuu ya Wilaya pale Manyoni. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuweza kukiimarisha Kituo hicho upya?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa tu ni kwamba barabara hiyo pia ndiyo hutumia Mheshimiwa Spika kwenda Jimboni Urambo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana tutahakikisha kwamba ulinzi upo na usalama mkubwa juu yako.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Mheshimiwa John Lwanji wakati wa ziara yetu tulipotembelea eneo hilo kwa namna ya makaribisho mazuri aliyotupa na ushirikiano mkubwa alionao kwa Jeshi la Polisi. Nataka niendelee tena kumhakikishia Mheshimiwa John Lwanji kwamba yale yote tuliyozungumza tunayafanyia kazi na tutahakikisha kwamba yale ya muhimu yote yanatekelezwa. Kama nilivyosema tatizo letu kubwa kwa sasa hivi ni ufinyu wa Bajeti. Lakini Serikali ina mpango mahsusi wa kuangalia uwezekano wa kujenga Vituo vya Polisi mbalimbali nchini. Kwa hiyo, naomba avute subira ili tuweze kufanikiwa katika mambo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi likiwemo la usafiri na mambo mengine muhimu kwa

Jeshi letu la Polisi. Nawaomba sana wananchi waendelee kusubiri wakati Serikali inatafuta utatuzi wa matatizo hayo. *(Makofi)*

Na. 190

**Kuanzishwa kwa SADC Brigade**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ni Mwanachama wa *SADC;* na kwa kuwa, jitihada za kuanzishwa *SADC Brigade* kwa ajili ya usalama wa nchi wanachama kwa kutatua matatizo na majanga ya nchi hizo zinaendelee vizuri:-

Je, kuna chombo chochote cha kidemokrasia kitachokuwa kinafanya kazi ya *Budget Management Oversight* ya itakayokuwa *SADC Brigade?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF A. IDDI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *SADC Standby* Brigade ilizinduliwa rasmi tarehe 17 Agosti, 2007, Mjini Lusaka, Zambia wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Serikali wa *SADC.* Uzinduzi ulifanyika baada ya viongozi wa Nchi 14 za *SADC* kuweka saini makubaliano ya uanzishwaji wa *Brigade* ya *SADC* yanayojulikana kama *Memorandum of Understanding Amongst the Southern African Development Community Member States on the Establishment of A Southern African Development Community Standby Brigade.* Makubaliano haya ndiyo yanayoweka misingi na taratibu za kisheria za kuanzisha na kuendesha *Brigade* ya *SADC.*

Mheshimiwa Spika, *SADC Standby Brigade* ilianzishwa kutokana na uamuzi wa umoja wa Afrika kuwa Jumuiya za Ushirikiano za Kanda ziwe na *Brigade* za kulinda amani. Kufuatia utaratibu huu wa umoja wa Kikanda, *Brigade* zote tano zimeshaanzishwa kama ifuatavyo:-

(i) Brigedi ya *SADC*;
(ii) Brigedi ya Mashariki inayojumuisha nchi zilizopo eneo la Mashariki mwa Afrika;
(iii) Brigedi ya Kati chini ya *Economic Community of Central Africa States (ECCAS);*
(iv) Brigedi ya Magharibi chini ya *Economic Community of West African States* (*ECOWAS*); na

(v) Brigedi ya Kaskazini inayoundwa na nchi za Kaskazini mwa Afrika.

Uamuzi wa kuanzishwa kwa Brigedi ya *SADC* ulipitishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* katika Mkutano wao uliofanyika Port Louis, Maurtius, tarehe 17 Agosti, 2004. Brigedi hii inajumuisha Jeshi, Polisi na Raia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kufuatia makubaliano ya kuanzisha Brigedi ya *SADC*, shughuli zote za kuendesha Brigedi ya *SADC* zinagharimiwa na *SADC* na usimamizi wa masuala yote ya kifedha unafanywa kwa kuzingatia Kanuni za Fedha za *SADC* (*SADC Financial Guidelines*).

Kwa misingi ya Mkataba wa *SADC* (*Treaty)*, masuala yote ya Bajeti, matumizi ya fedha na ukaguzi wa mahesabu husimamiwa na Baraza la Mawaziri wa *SADC* (*Council of Ministers*). Hiki ndicho chombo chenye Wawakilishi wa Nchi zote Wanachama kilichokabidhiwa jukumu hili.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa nia ya kuwa na *SADC* Brigedi ni kuwa na matakwa ya kiulinzi wa pamoja; na kwa kuwa viongozi wa nchi zetu wanajitahidi sana kuweka *security interest* ya nchi zetu pamoja lakini tunatofautiana katika sera zetu za kiulinzi wa nchi na nchi. Je, *SADC Countries* tumefikia wapi mkakati wa uundaji wa sera ya pamoja ili kuweza ku-*implement* na ku-*guide Common Defence and Security Interest?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF A. IDDI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli sera za nchi za *SADC* ya Ulinzi na Usalama ni tofauti, lakini utekelezaji wetu wa shughuli za ulinzi katika nchi za *SADC* inaongozwa na mikataba mbalimbali. Mfano mkataba wa Ushirikiano ambao unaweka bayana maeneo na madhumuni ya kushirikiana katika siasa, ulinzi na usalama.

Pia kuna itifaki ya siasa, ulinzi na usalama ambayo inaweka misingi ya kisheria ya Ushirikiano. Tatu yako makubaliano yaUshirikiano ya vyombo vya ulinzi *(SADC, Mutually, Defence, Packed)*. Nne, makubaliano yaliyowekwa saini *Memorandum of Understanding* ya kuanzisha Brigedi ya *SADC*. Makubaliano hayo yote yanatuongoza kwa pamoja katika utekelezaji wa ulinzi na usalama katika maeneo ya *SADC* na hata nje ya *SADC*.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi linauliza ni chombo gani cha kidemokrasia na duniani kote chombo kikubwa cha demokrasia kinachojishughulisha na *oversight* ni Bunge; na kwa kuwa katika Mkataba ulioanzisha *SADC Treaty* ya *SADC* ibara ya tisa (9) inazungumzia uanzishwaji wa Bunge la *SADC*; na kwa kuwa katika Kanda tano alizozungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri zote isipokuwa Kanda ya *SADC* haijaunda Bunge.

Je, ni nini kauli ya Serikali ya Tanzania sasa katika jitihada zinazofanyika kuunda Bunge la *SADC* kama Bunge halisi badala ya *forum* kama ilivyo sasa ili kufanya kazi ya *Oversight*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF A. IDDI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli *SADC* haijaunda Bunge, lakini mpaka sasa kuna tafakari ya kuanzisha chombo kama hicho hapo baadaye kidogo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa taarifa tu ya Serikali katika waanzilishi wa *SADC* ni sisi Tanzania peke yetu hatujaridhia uanzishwaji huo. Niliona nitoe taarifa kwa sababu huwa inanisumbua Maspika wenzangu wanaponiuliza hivi Tanzania vipi? Nadhani ni vizuri kulijua hilo. *(Makofi)*

Na. 191

**Kuwatumia Wafungwa Kuzalisha Mali**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi duniani kama China hutumia wafungwa kuzalisha mali kama vile kujenga reli, kufanya kazi viwandani, kulima mashamba na kadhalika:-

(a) Je, ni lini Serikali itawatumia wafungwa kuzalisha chakula chao kwa kulima mazao kama mahindi, maharagwe, alizeti, michikichi na kupanda miti kwa wingi ili kuipunguzia Serikali mzigo wa madeni na gharama za kuwalisha na kuwapa huduma mbalimbali?

(b) Je, kwa kuwaacha wafungwa bila kuzalisha mali wawapo Magerezani si kutumia rasilimali za Taifa vibaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi (Viti Maalum), lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wafungwa wenye makosa madogo madogo hutumika katika shughuli za uzalishaji mali kama vile ujenzi, uvuvi, kilimo cha mazao ya chakula

hususan mahindi, maharagwe, chai, kahawa, alizeti, michikichi na mazao yatokanayo na mifugo. Magereza yanayojishughulisha na kilimo cha mazao ni Songwe (Mbeya), Mollo (Rukwa), (Isupilo (Iringa), Arusha, Karanga (Kilimanjaro), Kwitanga na Ilagala (Kigoma) na Mng'aro (Tanga). Magereza yanayoshughulika na ufugaji ni pamoja na Kingolwira (Morogoro), Ubena Ranchi (Pwani), Mugumu (Mara na Kitengule (Kagera).

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Jeshi la Magereza linayo mashamba makubwa 49 kote nchini ambapo kati ya hayo, mashamba ya kilimo ni kumi na matatu (13), Ranchi za mifugo kumi na saba (17), mashamba ya ng'ombe wa maziwa ni mawili (2) na mashamba ya kilimo na mifugo (*mixed farming*) kumi na saba (17). Katika mashamba hayo, mashamba ya kilimo na mifugo 13 yapo chini ya Shirika la Magereza (*Prisons Corporation Sole*) ambapo yanaendeshwa kwa mtindo wa *Revolving Fund* kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Shirika hilo. Aidha, mashamba yaliyobaki huendeshwa na Jeshi la Magereza, kwa kupata fedha Serikalini kwa ajili ya kununua pembejeo na zana muhimu na mazao yapatikanayo huuzwa na fedha kuingizwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Jeshi la Magereza huwatumia wafungwa kwa shughuli za utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali ya Magereza ambapo hadi hivi sasa ekari 3,800 zimepandwa miti.

Mheshimiwa Spika, wafungwa wa vifungo virefu ambao hairuhusiwi kisheria kutoka nje kufanya shughuli za uzalishaji mali hufanya kazi za uzalishaji viwandani hususan kutengeneza samani, ushonaji nguo, utengenezaji viatu, ususi na uunganishaji vyuma. Shughuli zote hizi hufanyika kwa lengo la kuwarekebisha wafungwa na kuzalisha mali ili kuipunguzia mzigo Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na jibu nililotoa hapo ni dhahiri kuwa wafungwa wanatumika kuzalisha mali na suala la kutumia rasilimali za Taifa vibaya halipo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Kwa kuwa katika Magereza mengi kuna sifa kubwa sana ya utunzaji mzuri sana wa vifaa hasa magari na matrekta kuliko Idara nyingine za Serikali lakini baadhi ya Magereza kama Gereza la Kongwa halina vifaa vya uzalishaji mali wa kilimo kama matrekta lakini lina uwezo mkubwa sana wa kuzalisha mahindi mengi, maharagwe, alizeti ambayo yanaweza kutosha kulisha Magereza yote ya Mkoa wa Dodoma. Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema nini kuhusu kuliwezesha Gereza la Kongwa kuhusiana na vifaa vya kilimo hasa matrekta?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilishawahi kueleza Bunge lako Tukufu, Jeshi la Magereza hivi sasa linafanya tathmini ya Magereza yake yote ya kilimo hapa nchini ili kuamua ni Magereza yapi yapewe kipaumbele ili kupatiwa matrekta na vyanzo vingine vya kuweza kufanya

shughuli za kilimo. Tukimaliza tathmini hiyo tutaweza kujua kama Gereza la Kongwa linaweza likawa mojawapo ambalo litapatiwa trekta katika harakati za mwanzo. Lakini ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Jeshi la Magereza lina nia ya kuboresha shughuli za kilimo katika Magereza yake yote.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hata pale baadhi ya Magereza yanapozalisha chakula kingi kama vile Magereza ya Namteketa lililoko Nkasi na Gereza la Linamkulukulu lililoko Mpanda na mengineo, Magereza hayo huwa hayaruhusiwi kutumia chakula chake pale Gerezani mpaka chakula chote kiende Makao Makuu na wao ndipo wapewe mgao hata kama wanapata shida ya chakula. Je, utaratibu huo kwa nini upo na kwa vile ni utaratibu ambao nauona mimi sio mzuri kwa nini Magereza yale yasiruhusiwe kutumia chakula ambacho wamezalisha wao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Magereza yetu yanaruhusiwa kutumia chakula ambacho wanazalisha pale kwenye maeneo yao lakini huwa tuna utaratibu wa kukusanya mazao katika *centralised location* kwa sababu sio Magereza yote ambayo yanalima vyakula vyote unaweza ukakuta kwamba Gereza moja wana mahindi lakini hawana mpunga. Kwa hiyo, inabidi mazao haya yote yamekusanywa pamoja halafu tunayasambaza ili kukidhi mahitaji ya wafungwa katika Magereza yetu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tumekuwa tukitenga kiasi cha fedha kwa ajili bajeti ya chakula cha wafungwa na Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kuna mashamba haya 49, kwa nini tuendelee kupanga bajeti kwa asilimia mia moja kwa ajili ya chakula chao wakati wanalima wenyewe?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, mashamba yetu ya kilimo yamegawanywa katika maeneo mawili. Kuna Magereza *Corporation Sole* ambapo ni Shirika ambalo linajitegemea ndani ya Magereza, huwa linauza mazao yake kwa Magereza yetu na kuna Magereza yetu mengine ambayo yanazalisha kama nilivyoeleza ambapo yakizalishwa, fedha huwa inapelekwa Serikali Kuu. Ina maana kwamba hata kama Magereza yakizalisha, Serikali inabidi kununua kutoka kwenye Magereza *Corporation Sole* na hili ni suala la *accounting* na haliwezi kuepukika.

Na. 192

**Barabara ya Marangu –Tarakea**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Marangu – Tarakea ipo kwenye maandalizi ya ujenzi na kwa kuwa, Marangu Mtoni mahali ambapo barabara inaanzia ni kituo kikubwa cha mabasi yaendayo Moshi, Rombo, Kilema na Kilimanjaro *National Park*:-

Je, Serikali ipo tayari kuipanua barabara hiyo kutoka eneo hilo na kuimarisha kituo hicho cha mabasi wakati wa ujenzi wa barabara ya Marangu – Tarakea?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi hasa ukizingatia wingi wa magari yaendayo Moshi, Rombo, Kilema na *Kilimanjaro National Park*. Lakini kutokana na hali halisi ya mji mdogo wa Marangu Mtoni ulivyo ambapo upande mmoja kuna mto na upande mwingine kuna majengo ya gharama kubwa, inakuwa ni vigumu kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi.

Aidha, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Marangu - Rombo Mkuu ambao utekelezaji wake unaendelea, hauhusishi ujenzi wa kituo cha mabasi kinachopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge. Kutokana na ukweli huu, itakuwa vigumu kujumuisha ujenzi wa kituo cha mabasi katika mradi unaoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, itaangalia uwezekano wa kupata eneo mbadala kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi na kuona pia uwezekano wa kupanua barabara hiyo katika eneo hilo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kuwepo kwa wingi wa magari yaendayo *Kilimanjaro National Park*, Rombo, Kilema na baada ya ujenzi wa barabara hiyo magari yaendayo Nairobi yataongezeka kwa sababu yatakuwa yanapita njia hiyo, je, kwa kuwa kuna soko pale na soko hilo lina eneo la kutosha kujenga stendi, Serikali haioni ni muhimu hasa kuangalia usalama wa raia wake kwa kujenga stendi nusu ya eneo la soko hilo?

(b) Kwa kuwa ujenzi wa barabara ambayo itakwenda Kilema pamoja na Kirua aliyoahidi Mheshimiwa Rais, unaanzia Marangu Mtoni, je, Serikali inaweza kueleza mpaka sasa hivi maandalizi yake yamefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye umuhimu wa soko kama alivyozungumza. Lakini nadhani yeye ni Mjumbe wa Halmashauri, wakae waamue kwenye Halmashauri umuhimu wa kujenga hilo soko katika eneo lililopangwa kama wanavyotaka wao. Kama watamega au watatafuta eneo lingine, ni maamuzi ambayo yapo katika mikono yao.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya kujenga barabara ya Kilema, Kirua iko pale pale na maandalizi ya ujenzi, yanaendelea kama yalivyopangwa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kutenga kiwango cha fedha kama Sh.4.6 bilioni kwa ajili ya barabara za Tarime. Barabara ya Tarime - Nyamwaga imeharibika kwa muda wa miaka mingi na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi juzi alikuja ameona mwenyewe adha wananchi wanayoipata na wakampa kilio chao.

Sasa naomba kuuliza kwa nini mpaka sasa haijaanza kulimwa wakati fedha zimeshatolewa na Serikali na kile kipande cha kilomita 2 ambacho kimewekwa lami hakiendi kwa viwango? Naomba nipate jibu.

**SPIKA:** Majibu, ingawa limehamia katika sehemu nyingine lakini pengine Mheshimiwa Naibu Waziri unayo taarifa.

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge alilete kwa sababu suala la msingi halihusiani na barabara ya Tarime, akilileta kama ni suala linalohitaji majibu, basi tutalifanyia kazi.

Na. 193

**Ujenzi wa Barabara ya Iringa –Dodoma - Babati**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kujenga barabara ya Iringa – Dodoma - Babati kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, Serikali inajiandaa vipi kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imejiandaa kutekeleza ahadi yake kwa kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na hatimaye usanifu wa kina kwa barabara ya Iringa – Dodoma -Babati. Ili kuharakisha utekelezaji wa ahadi hiyo, barabara ya Iringa - Dodoma - Babati imegawanywa sehemu mbili ambazo ni Iringa - Dodoma na Dodoma - Babati na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Iringa - Dodoma:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Iringa - Dodoma ulisainiwa tarehe 22/08/2007 kati ya *TANROADS* na Kampuni ya Kihandisi ya *Cowl Consult*. Kazi hii inafadhiliwa na *Nordic Development Fund (NDF)* na usanifu utachukua miezi 18.

(ii) Dodoma - Babati:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa barabara hii unafanywa na Kampuni ya *Carl Bro* ya Denmark. Kazi hii inagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na mkopo kutoka *Nordic Development Fund (NDF)* na Benki ya Dunia. Kazi ya usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2008.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Iringa - Dodoma - Babati kwa kiwango cha lami, utaanza baada ya kukamilishwa kwa usanifu wa kina na upatikanaji wa fedha za ujenzi wa barabara hiyo. Aidha, wakati kazi ya usanifu wa kina ikiendelea, Serikali inaendelea kuwasiliana na Wahisani mbalimbali ili kupata fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa usanifu wa kina wa barabara kati ya Dodoma na Babati karibu unakamilika na kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba wanatafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami lakini wafadhili hao kwa muda wa miaka 30 iliyopita hawajawahi kupatikana, je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kutenga fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa barabara kati ya Dodoma na Babati?

(b) Kwa kuwa hivi sasa Serikali iko katika mchakato wa kuzungumza na Serikali ya Marekati kupitia *MCC* na kwa kuwa Serikali ya Marekani imeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba ni vema barabara ya Dodoma - Babati ingewekwa katika mradi huu wa *MCC*?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba wafadhili wanachukua miaka 30 bila kupata matokeo. Wakati natoa majibu haya, wako wafadhili ambao wamesaidia hata katika usanifu na *feasibility study* ya barabara zetu nyingi na ni wafadhili hao hao ambao wanatusaidia katika barabara mbalimbali hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali inafanya juhudi ya kutafuta wafadhili. Tuna hakika, mwakani barabara hizi zitawekwa katika mpango wa matengenezo kama tunavyofanya siku zote.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango hii ya Serikali kwa barabara hii ya Dodoma kwenda Babati, kuna kero moja kubwa ya barabara hii, kilomita chache kabla hujafika Kolo kuna daraja kubwa ambalo limevunjika na limekaa pale kwa miaka mingi sana. Je, ujengaji wa daraja hili nao utasubiri ukamilishaji wa usanifu au inakuwaje maana ni kero kubwa na magari yanapita mtoni pale na ni hatari nyakati za mvua?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutamtaka *Regional Manager* wa *TANROADS* wa Dodoma aende akaliangalie hilo daraja ili aone namna gani anaweza kufanya marekebisho hayo.

**SPIKA:** Ahsante sana, hili ndilo jibu la kasi mpya.

Na. 194

**Hitaji la Hakimu wa Mahakama**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imejenga Mahakama ya Mwanzo kwenye Kata ya Lituhi ambayo ni nzuri sana na ya kisasa na kwa kuwa, Kata hiyo imekosa huduma kwa takriban miaka ishirini (20) baada ya wananchi hao kuhamishwa na baadaye mwaka 1986 kurejeshwa na Serikali:-

Je, ni lini Mahakama hiyo itapatiwa Hakimu wa kudumu wa kuwahudumia wananchi wapatao elfu kumi na mbili (12,000) badala ya kuazimwa Hakimu toka Kata ya jirani anayekaa umbali wa kilomita thelathini na tano (35 km)?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa Mahakama ya Mwanzo, Lituhi, Mbinga, haina Hakimu wa kudumu bali hutembelewa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kutoka Mahakama ya Ruanda. Hali hii inatokana na uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo uliopo katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tunazo Mahakama za Mwanzo 1,105 nchi nzima, lakini Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo waliopo ni 509 tu. Kwa upande wa Wilaya ya Mbinga, tunazo Mahakama za Mwanzo 14 na ina Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 7. Kutokana na upungufu huu, ni dhahiri sio Mahakama zote za Mwanzo zina Mahakimu wa Kudumu. Ili kusogeza huduma ya Mahakama kwa wananchi, inabidi Mahakama zingine kutembelewa kama hiyo ya Lituhi. Mahakama imeendelea kupanua mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika vyuo vya Lushoto na Mzumbe ili kukidhi mahitaji ya Mahakimu nchini.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira pindi tutakapopata Mahakimu wa kutosha, Mahakama ya Lituhi itapelekewa Hakimu wa kudumu ili wananchi wa Mbinga wapate huduma hiyo kwa karibu zaidi.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa sasa pale Lituhi, kesi nyingi zimerundikana, je, Serikali ina mpango gani wa kumuamuru yule Hakimu abaki pale Lituhi kwa muda mrefu ili amalize kesi zile?

(b) Kwa kuwa jengo lenyewe lina thamani kubwa na wako vibaka na wezi wanavizia kuiba vioo na milango, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ulinzi na utunzaji wa jengo lenyewe?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nalichukua ombi la Mheshimiwa Mbunge na kuona uwezekano wa Hakimu kukaa muda mrefu zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wizi wa vifaa, nitajaribu kuwasiliana na Mahakama ya Tanzania, ili kuona tunachukua hatua zipi ili wizi huo usitokee.

Na. 195

**Adhabu ya Kifo**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

(a) Je, mama mjamzito anaweza akahukumiwa adhabu ya kifo kama amepatikana na hatia?

(b) Kama jibu ni ndiyo, je, hukumu hiyo haiwezi kumwathiri mtoto aliye tumboni?

(c) Je, kwa nini Serikali isiifute adhabu hiyo kwa kuwa inarudia kufanya kosa hilo hilo la mauaji?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwia Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, adhabu ya kifo kisheria inapaswa kutolewa kwa mtu yeyote anayepatikana na hatia kwa kosa la kuua kwa kukusudia chini ya vifungu 196 na 197 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha Sheria hiyo, adhabu ya kifo haitolewi kwa mwanamke atakayedhihirika kwamba yeye ni mjamzito. Badala yake, mwanamke huyo atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la sehemu (a), kwa kuwa mwanamke mjamzito hapewi adhabu ya kifo, adhabu hiyo haiwezi kumuathiri mtoto wake aliyepo tumboni.

(c) Mheshimiwa Spika, adhabu ya kifo bado ni adhabu halali kwa Tanzania. Hata hivyo, ili kujiridhisha kama bado adhabu hii inafaa kwa wakati tulionao, Serikali imeiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kupata maoni ya wananchi walio wengi ili kuona kama jamii bado inaihitaji. Serikali itafanya tathmini kama kweli sasa ni wakati muafaka wa kuifuta adhabu hii, baada ya kupokea matokeo ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na kwa kupitia Bunge lako Tukufu, niwaombe wananchi wote kutoa ushirikiano kwa Tume ya Kurekebisha Sheria ili kufanikisha utafiti huo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo pia yametoa elimu kwa sisi wote hapa. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika taarifa nilizozipata kutoka kwa wataalamu wa masuala ya akinamama, inasemekana mama mjamzito anapata mchemko wa kisaikolojia anapokuwa yuko katika hali hiyo na kwa kuwa bado atahitajika kutumikia adhabu ya kifungo cha maisha je, Serikali haioni ni vyema ikaangalia pia uwezekano wa kupunguza adhabu hii?

(b) Kwa kuwa sasa hivi karibu katika magazeti ya kila siku, utaona hali ya ugomvi na kuuana katika familia inazidi kuongezeka, je, Serikali inachukua hatua gani ya kuweza kuweka vituo vya kuweza kutoa ushauri wa kifamilia ili kuweza kupunguza matatizo hayo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa vyote vyote vile mama mjamzito anapojikuta kwenye hali ya kufungwa atakuwa na athari za kiafya. Katika kumlinda motto, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi hukumu ya kifo inaondolewa lakini kwa kujali haki ya upande ule mwingine, itakuwa vigumu sana kumwondolea adhabu hiyo ya kifungo cha maisha. Lakini ni mawazo aliyoyatoa ni mazuri nafikiri Serikali itachukua hatua ya kufuatilia na kuona nini kiweze kufanyika ili kuweza kuona haki inatendeka kwa pande zote mbili.

Kuhusu swali lake la pili, nakubaliana na namshukuru sana kuleta wazo hili zuri. Kutokana na matukio ya hivi sasa kwamba pengine pamekosekana amani ndani ya familia na pengine ni muda muafaka wa kuanzisha vituo vya ushauri nasaha kwa ajili ya familia. Hilo litachukuliwa na Serikali na jamii kwa ujumla tuone tunafanya nini kwa sababu chimbuko la amani ya Tanzania linatokana na familia zetu.

**MHE. DR. ZAINAB M. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali inakuwa na huruma sana kwa kumwadhibu huyu mtoto aliyekuwa tumboni kwa adhabu ya kifo kwa hiyo ikampa mama adhabu ya kifungo cha maisha. Je, Serikali inaandaaje huruma hiyo hiyo huyu mtoto aliyekuwa tumboni asifungwe kifungo cha maisha kama alivyofungwa mama yake?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kutokana na sio huruma tu ni haki ya mtoto ambaye yuko tumboni kuishi na ndiyo maana basi mama hapewi adhabu ya kifo na ndiyo maana adhabu ikapunguzwa kuwa adhabu ya kifungo cha maisha ili kusudi mtoto huyo asiathirike kwa kifo cha mama yake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mtoto ambaye yuko tumboni hana hatia na si haki yake kufungwa, lakini kwa sababu ni lazima awe na mama yake, inabidi iwe hivyo. Lakini ningependa kuishauri familia au ndugu wa karibu kama wanaweza wakati mtoto akiacha kunyonya basi kumchukua ili kusudi mtoto huyo asijikute yuko Gerezani.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuulizwa swali. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ziko fomu ambazo wakati mwingine mtu anatakiwa kujaza kujieleza kama amefungwa au hajafungwa, je, mtoto aliyezaliwa jela akiulizwa kama alifungwa ama hakufungwa, atatakiwa kujibu kwamba amefungwa kwa sababu ya mama yake? (*Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambalo limefurahisha watu wengi humu Bungeni, namshukuru sana kwa pongezi zake. Adhabu iliyotolewa kwa mama, haimuhusu mtoto na kwa hivyo wakati wowote kwenye maisha yake hatajikuta anajibu kama amefungwa kwa sababu hajawahi kuhukumiwa. Lakini ni kweli kabisa mama anapofungwa, mtoto anapokaa jela na yeye hapati uhuru na maelezi ambayo angeyapata akiwa nje. Ndiyo maana nasisitiza kwamba atakapokuwa ameacha kunyonya, basi ni vizuri wale ndugu waliokaribu kama baba, shangazi na wengine basi waweze kumchukua mtoto huyo ili aweze kukaa mahali ambapo pana heshima kuliko jela.

Na. 196

**Kupeleka Umeme – Vijiji vya Wilaya ya Mkinga**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Daluni Gombero, Kwale na Mkinga, Wilayani Mkinga walipata matumaini makubwa ya kuwekewa umeme na Serikali mwaka 2003 na kwa kuwa hivi sasa tayari maandalizi ya uundaji wa Mfuko wa Umeme vijijini na Shirika la Umeme uko katika hatua za mwisho:-

(a) Je, wananchi wa vijiji nilivyovitaja watarajie kupatiwa umeme katika siku za hivi karibuni?

(b) Je, ni lini umeme uliofikishwa kwa nguzo na waya hadi kijiji cha Mkinga unatazamiwa kuwekewa transfoma na vifaa vingine ili taasisi kama vile shule zahanati viweze kutumia umeme huo?

(c) Je, ni lini Kasera, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, itapatiwa umeme ama kutoka taasisi jirani au kutoka 33 *KV line* inayopita katikati ya kijiji cha Kasera kutoka Tanga kwenda Mombasa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga ,lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(b) Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kuwapatia umeme wananchi wa vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale, zimepata mafanikio kwa vijiji hivi kuwekwa kwenye mpango wa kusambaza umeme unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millenium Challenge Corparation* (*MCC*).

Gharama za kupeleka umeme kijiji cha Dulima ni shilingi 162,239,191/= ambayo inajumuisha ujenzi wa kilomita 10 za njia ya Kilovolti 11, transforma ya *KVA 50* na njia ndogo ya msongo wa volti 230/400 zenye urefu wa kilomita 2.

Kazi ya kupeleka umeme kijiji cha Gombero inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 33 umbali wa kilomita 19, uwekaji wa transforma 2 za ukubwa wa *KVA* na ujenzi wa njia ndogo za umeme za msongo wa volti 230/400 za urefu wa kilomita 2. Jumla ya gharama zote ni shilingi 292,564,092/-

Gharama za kupeleka umeme kijiji cha Kwale ni shilingi milioni 243,664,006/-. Utekelezaji wa mradi huu utahusisha ujenzi wa kilomita 7 za njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 33, ufungaji wa transfoma moja ya ukubwa wa *KVA 50* na ujenzi wa njia ndogo za msongo wa volti 230/400 yenye urefu wa kilomiya 15.

(b) Mheshimiwa Spika, njia ya umeme iliyojengwa katika kijiji cha Mkinga imekwishafungwa transfoma hivyo kijiji pamoja na zahanati ya kijiji hicho tayari wana huduma ya umeme na wanatumia umeme kwa hivi sasa.

(c) Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga (Kasera) yatapitiwa umeme kutoka katika njia ya umeme wa msongo wa Kilovolti 33 itokayo Tanga kwenda Horohoro hadi Mombasa. Gharama za kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga ni shilingi 63,203,977.00. Utekelezaji wa mradi huu utaanza mwaka huu wa fedha.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu fasaha na yenye kuleta matumaini. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kuhusu Makao Makuu wa Wilaya ya Mkinga, napenda kueleza kwamba malipo tayari yameshafanyika na hivi sasa majengo ya Makao Makuu ya Wilaya hiyo yamekamilika yanasubiri umeme tu uunganishwe ili waweze kuhamia. Sasa je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutufahamisha ni lini hasa umeme huo utaunganishwa ili yaweze kutumika haraka iwezekanavyo?

(b) Nimepata matumaini mazuri kusikia kwamba vijiji vya Daluni, Gombelo na Kwale vimo katika mpango kamambe wa kupatiwa umeme chini ya ufadhili wa *MCC*. Kwa kuwa maombi hayo yamekuwa ya muda mrefu sana je, si vizuri Waziri akatoa ufafanuzi ni lini unatazamiwa umeme kufika huko?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, umeme wa kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kama nilivyosema, tunatarajia tuanze kushughulikia mwaka huu na hii inatokana na kifungu cha fedha ambacho tumepata ambacho sana sana kimelenga kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya kama tulivyoahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na sasa hivi mpango unafanywa kwa sababu si sehemu hii peke yake ni sehemu nyingi ambazo tumezipanga ambazo zinahitaji kupeleka Makao Makuu ya Wilaya na hii ya Mkingi ikiwemo. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tunatarajia mwaka huu umeme utafika. Katika Mpango wa *Millenium Challenge Account (MCCA)*, kama mnavyofahamu, ndiyo imepitishwa katika taratibu za Kimarekani na sasa hivi tunatengeneza mipango ya usimamizi wa utaratibu huu kwa hapa Tanzania na tukishakamilisha, tutawatangazia hapa Bungeni ili Bunge lako Tukufu liweze kufuatilia utekelezaji wake.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga linafanana sana na suala zima la kupeleka umeme katika Makao Mkuu ya Wilaya ya Songea, Mkoani Ruvuma na mpaka Makao Makuu ya Jimbo la Peramiho, kule Peramiho, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kutuambia ni kiasi gani mradi huo wa umeme umeshaanza kutekelezwa ili wananchi wa Songea Mjini na kule Peramiho wapate matumaini kwamba sasa umeme unakaribia kufika kwao?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tuna mpango kabambe ambao unapeleka umeme wa gridi Mikoa ya Kusini ambao utatoka Makambako, Songea mpaka Mbinga. Sasa hivi, mchakato umeshafanyika na unatagemea kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya *SIDA* ya Serikali la Sweden. Mpaka sasa hivi mipango yote ambayo inafadhiliwa na Serikali ya Sweden, inategemea kupitishwa katika vikao vyao ambavyo tunatarajia watakuwa wamekaa mwezi huu wa kumi na moja na Wizara yangu inafuatilia pindi tu baada ya kukamilisha taratibu zao, tutawaeleza Waheshimiwa Wabunge na ikiwezekana tutalieleza Bunge kwenye kikao kijacho cha mwezi wa pili kwa sababu hii miradi yote iko sehemu nyingi Tanzania na inafadhiliwa na Shirika la *SIDA*.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na swali linalofuata linaloekezwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ninatoa ushauri tu kwa Wizara hii kwamba tafsiri ya kufikisha umeme usiwe kama ile ya Urambo, kwamba umeme ukifika Bomani ndiyo tayari, ingezingatia pia kuusambaza umeme ili kuwe na tija.

Na. 197

**Tatizo la UKIMWI Nchini**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI yanazidi kuendelea siku hadi siku nchini, jambo ambalo ni tofauti kwa nchi nyingine ambapo maambukizi yanapungua kwa asilimia kubwa:-

(a) Je, Serikali inafahamu na kuzingatia njia wanazotuma nchi nyingine ili nasi tufaidike nazo?

(b) Je, Serikali kufanya semina za umma mara kwa mara na kugawa vipeperushi ndilo suluhisho la kutokomeza UKIMWI au ni njia ya kuwafanya wahusika kuwa wagumu na waoga wa kupima na hivyo kuendelea kufanya maambukizi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, viwango vya maambukizi ya virusi vya UKIMWI hapa nchini. vinaonyesha mwelekeo wa kushuka. Utafiti uliofanywa na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini kote kwa kupima viwango vya maambukizi miongoni mwa akina mama wajawazito katika miaka tofauti, umeonyesha viwango vifuatavyo:-

Mwaka 2001/2002 asilimia 9.7, mwaka 2002/2003 asilimia 8.7 na mwaka 2005/2006 asilimia 8.2. Takwimu hizi ni kielelezo thabiti kuwa viwango vinashuka na tutaendelea kuvifuatilia.

Aidha katika kituo chetu cha Kagera ambapo ndipo UKIMWI ulitambuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1983, kuna dalili za wazi kabisa kuwa viwango vinashuka kama ifuatavyo:-

| Mwaka | Viwango vya Maambukizi |
|---|---|
| 1990 | 22.2% |
| 1994 | 17.3% |
| 2000 | 12.5% |
| 2004 | 9.5% |
| 2005 | 5.8% |

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inafahamu na kuzingatia njia za kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI wanazotumia nchi nyingine. Njia hizo ni pamoja na:-

- Kutoa damu;

- Kuhakikisha usalama wa damu wanayoongezewa wagonjwa hospitalini;

- Kutibu magonjwa ya ngono;

- Kudhibiti maambukizi ya virusi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto;

- Kutoa ushauri nasaha na upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI;

- Kusambaza dawa za kupunguza makali ya UKIMWI na kutoahuduma za mafunzo kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI; na

- Kusambaza mipira ya *condom*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa njia zote nilizozitaja hapo juu zinatumika pia hapa nchini na kwa kweli tumefaidika nazo kwa kupunguza kiasi cha maambukizi ya UKIMWI kama nilivyoelezwa katika utangulizi.

(b) Kufanya Semina mara kwa mara na kugawa vipeperushi ni sehemu tu ya mikakati inayotumika katika kudhibiti UKIMWI kama ilivyoelezwa katika kipengele (a). Semina zinatolewa kuwapa mafunzo watumishi wa afya ili kuwawezesha kutoa huduma zilizobora za kudhibiti UKIMWI. Kwa upande wa mwingine, vipeperushi hugawiwa ili kusambaza habari na ujumbe mbalimbali kuhusu huduma zinazopatikana katika kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha wananchi kwamba ugonjwa huu wa UKIMWI bado haujapatiwa dawa wala chanjo. Dawa aina ya *ARV's* zinapatikana na zinazotolewa bure kwa wale wanaostahili lakini hazina uwezo wa kuponyesha. Kwa hiyo, tukitaka kushinda katika pambano hili dhidi ya UKIMWI na tumedhamiria kushinda ni lazima tuwakinge wananchi ambao bado hawajapata maambukizo ili wasipate hayo maambukizo. Silaha kuu ya kutimiza azma hiyo, ni wananchi kubadili tabia na njia ya kuwafanya wabadili tabia ni kuwapa elimu. Semina, vipeperushi, ujumbe katika mabango, radio, televisheni, michezo ya kuigiza na kadhalika, ni njia zinazotumika kueneza elimu hiyo kote duniani.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na kuwa kigezo kilichotumika ni kuwa Mkoa wa Kagara unaendelea kupungua kwa maambukizi je, Serikali imeangalia vituo vile ambavyo vinaendelea kuongezeka kwa maambukizi zaidi hapa nchini?

(b) Pamoja na kampeni zinazofanyika za kupunguza maambukizi ya UKIMWI lakini bado wapo wananchi ambao hawapendi kujitokeza kupima na wala hawana nia ya kupima kabisa na wanaendelea kuambukiza ugonjwa huu kwa vijiji ambavyo hawajulikani, je, Serikali inachukua hatua gani kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, nilipokuwa nazungumzia suala la Kagera, nilikuwa natoa mfano tu ili kuweza kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge jinsi gani tumepunguza UKIMWI hapa nchini. Lakini kama nilivyoeleza katika utangulizi wangu kwamba tathmini iliyofanywa na Programu ya Kupambana na UKIMWI imeonyesha kwa asilimia kubwa kwamba maambukizi ya virusi vya UKIMWI inaongezeka. Kwa hiyo, kuitaja Kagera nilitoa tu mfano ukilinganisha na zile takwimu ambazo nilizitoa katika jibu langu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kabisa kwamba kampeni zinafanyika na watu hawapendi kujitokeza na wanaendelea kufanya maambukizo ya makusudi. Kama tunavyofahamu wote, Serikali inafanya jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba kampeni ya kudhibiti UKIMWI inaendelea na kama tunakumbuka tarehe 14 Julai, 2007, Mheshimiwa Rais alizindua kampeni hii ya kupima kwa hiari kule Dar es Salaam kampeni ambayo inaendelea mpaka Desemba. Lakini vile vile, kwa wale ambao wanaambukiza, hawataki kupima na vilevile wanasambaza kwa makusudi virusi ya UKIMWI, sheria inafanyiwa maandalizi na itaeletwa hapa Bungeni baada ya wananchi kutoa maoni yao na sisi hapa tutaiangalia na kupitisha sheria hiyo ili waweze kubanwa na kuchukuliwa hatua zinazostahili.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pamoja na majibu yote mazuri na kwa kuwa imeonekana watu wanaambukizana kwa makusudi, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa hivi wale wanaopimwa na kupatikana na UKIMWI, wawekewe alama ama muhuri ili kuondokana na tatizo hili la kuambukiza kwa maksudi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la kupima na suala la kutambua wale wenye virusi vya UKIMWI, sera na sheria yetu kama tulivyosema, ni upimaji wa hiari. Nilipojibu swali la Mheshimiwa Maida, nimesema sheria inaandaliwa. Lakini wale wanaojitokeza na kupimwa wakaonekana na UKIMWI, mimi naona si busara kuwawekea alama kwa sababu kuwawekea alama ni njia mojawapo ambayo tunaonyesha kwamba tunawanyanyapaa. Sisi hapa tunapiga vita unyanyapaaji wa wagonjwa hao wa UKIMWI kwa sababu waliopata ugonjwa huu wameupata kwa njia tofauti. Kwa hiyo, kumweka alama ama muhuri, kwa kweli huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Yono, kwamba tusiendekeze suala hili kwa sababu tutakuwa tunaendekeza unyanyapaa lakini nitoe wito kwa wananchi tuendeleee kuwapenda wagonjwa wa UKIMWI kwa sababu wagonjwa hawa wanahitaji faraja na wanaweza wakaishi kama watu wengine na kuchangia maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla badala ya kuwatia mihuri na kuwanyanyapaa.

Na. 198

**Kuongeza Mtaji wa Benki ya Rasilimali (*TIB*)**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ilisema kuwa inatarajia kuongeza mtaji wa Benki ya Rasilimali kwa madhumuni ya kuiwezesha benki hiyo kutoa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu hususan katika sekta ya kilimo na viwanda:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza azma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana sana kimaudhui na swali Na. 90 la Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mbunge wa Mfenesini, tulilojibu tarahe 7/11/2007. Hivyo, kama nilivyosema wakati najibu swali hilo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mnamo mwaka 2005, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) iligeuzwa kuwa Benki ya Maendeleo kwa ajili ya kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa sekta ya uzalishaji hapa nchini, ambapo ilikubalika kwamba mtaji wa benki hii uwe Tsh.50.0 bilioni. Katika hatua za awali, mnamo mwaka 2006, Serikali iliidhinisha *TIB* kutumia kiasi cha Tsh.12.7 bilioni kutokana na Mradi wa Kukarabati Vituo vya Petroli (*Petroleum Sector Rehabilitation Project PSRP*) kuwa mtaji.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeongeza mtaji wa *TIB* kutoka Sh.7.721 bilioni hadi Sh.24.9 bilioni. Hatua inayofuata ni Serikali kuuza hisa zake katika *Tanzania Development Finance Limited (TDFL)* ambapo mapato yake pia yataongezea mtaji wa Serikali katika *TIB*. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti ya Serikali kwa awamu ili kuhakikisha kuwa kiwango cha mtaji cha Tsh.50.0 bilioni kilichokubaliwa kinafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoahidi wakati tunajibu hoja ya Mheshimiwa Shellukindo kuhusu *TIB*, Serikali itafanya majadiliano na Benki Kuu ya Tanzania, *PPF*, *NSSF*, *PSPF* na *LAPF*, kuona kama mashirika haya yanaweza kuwekeza mtaji kwa namna ya hisa katika Benki hiyo ili kiwango cha shilingi bilioni 50 kifikiwe mapema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii, Serikali imeruhusu *TIB* kuwezesha kukopa kiasi cha *USD5.0* milioni kutoka nje ya nchi kwa lengo la kupata fedha za kutoa

mikopo kwa wawekezaji wa kati (*SMEs*) ikiwa ni njia mojawapo ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu mazuri lakini nina maswali yafuatayo ya nyongeza. Kwanza, nataka nisisitize kwamba bila mikopo ya muda mrefu na wa kati, kasi ya ukuaji wa uchumi wetu itaendelea kuwa inalegalega. Baada ya kusema hivyo, nataka Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie. Hisa ambazo Serikali itauza kule *TDFL* ni kiasi gani na zitapatikana lini?

Lakini la pili, natoa ushauri. Serikali inaweza kwa urahisi zaidi kuwekeza kwenye Benki hii kwa kuuza *long term bonds*. Mashirika aliyoyataja ni mashirika ya kibiashara. Benki yoyote ya maendeleo si benki ya biashara, mashirika haya aliyoyataja hayawezi kuwekeza kwa sababu si mahali pa biashara. Kwa hiyo, huu ni mzigo wa Serikali na Serikali iubebe iuze *bonds* za muda mrefu halafu iwekeze kwenye hii benki. Sijui Serikali inachukuaji ushauri huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba ipo haja ya kuwa na chombo cha kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu na katika jibu langu la msingi, tumesema hivyo na kwamba tunaifanyia uchambuzi *TIB* ili kufanikisha hilo.

Wakati najibu swali la Mheshimiwa Shellukindo wakati akipendekeza kwamba iundwe Benki ya Kilimo, nadhani tulilijibu kwa ufasaha kabisa kwamba tulilichukua ombi lake na kulifanyia kazi na ikiwezekana kabla ya mwaka ujao wa fedha tuwe tumekuja na mapendekezo ya kuunda chombo ambacho kinaweza kikatoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu. Kuhusu hisa ambazo tunategemea kuuza *TDFL,* tunategemea kupata kati ya shilingi bilioni 10 na bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *long terms bonds*, Serikali haiwezi kukataa ushauri huo, tunakubaliana nao, tutaushughulikia.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa nchi nyingi duniani zina benki hizi za maendeleo na kwa kuwa wengi wetu tunatambua kwamba tulikuwa na benki kama hiyo *TRDB* wakati huo. Je, Serikali haioni umuhimu hata wa kuibadilisha benki hiyo hata kwa jina tu ielekee kwenye muelekeo wa maendeleo kuliko *TIB* ilivyo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli *TRDB* ilikuwa Benki ya Maendeleo. Tuliondoa msisitizo wa *rural* tukaweka msisitizo wa *co-operative.* Kwa hiyo, ikabadilishwa jina kutoka *Tanzania Rural Development Bank* kwenda *Cooperative and Rural Development Bank. CRDB* ni Benki ambayo inatoa mikopo ya maendeleo lakini kwa masharti ambayo

wanayo wao. Tunakusudia kulirekebisha *in fact* limesharekebishwa, *TIB* imesharekebisha kinachogomba hapa mtaji hautoshi. Kwa hiyo, *TIB* tuliyonayo sasa hivi ni *actually* Benki ya Maendeleo lakini mtaji uliopo wa shilingi bilioni 24.9 hautoshi. Kwa hiyo, msingi wa swali zima ni kwamba mtaji ule uongezwe na kwa mtazamo wa Mheshimiwa Juma Kaboyonga uongezwe haraka na Serikali tunakubali kwamba tutaongeza haraka. Kwa hivyo, Benki ya Maendeleo kwa kweli tayari tunayo tatizo pesa kupatikana haraka ili *TIB* iweze kutoa mikopo mikubwa ya muda mrefu na muda wa kati. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, tutaanza na matangazo. Tutaanza na wageni. Mheshimiwa Kapteni Chiligati, Waziri wa Kazi, ana viongozi wa CCM, Kata ya Chikuyu, Manyoni ambao wanaongozwa na Diwani wa Kata hiyo, Mheshimiwa Margaret Ndaga, naomba Mheshimiwa Margaret na wageni wengine msimame. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wale mliokuwapo Bungeni zamani, mtamkumbuka Mheshimiwa Margreth Ndaga alikuwa Mbunge mwenzetu. Baadaye akateuliwa na Rais kuwa *DC* kwa muda mrefu na sasa amestaafu. Lakini siasa si rahisi kustaafu moja kwa moja, kwa hiyo sasa ni Diwani. Asante sana! *(Makofi)*

Mheshimkwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ana mgeni wake ambaye ni ndugu Suleiman Nyamvi, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Songea. Yule pale, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fuya Kimbita anao wageni kutoka *TAG* Hai Mjini wanaongozwa na Mchungaji Evagast Solomon Swai. Wageni wa kutoka Hai, karibuni sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kutoka Mkoa wa Mara, wanao wageni wao ambao ni Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya na Madiwani kutoka Mkoa wa Mara wakiwa 25 wakiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Joseph Malimbe, Mwenyekiti wa *ALART* Mkoa wa Mara. Naomba Madiwani wa Mara tafadhali! Wale pale! Karibuni sana! *(Makofi)*

Wakati huo huo, nitangaze kipekee, Mheshimiwa Chacha Wangwe (ili wasiwe wameachwa hawa kwa sababu hawa ni Madiwani wa Kambi ya Upinzani), Ndugu Charles Mwera Nyangulu, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na Madiwani wenzake: Mheshimiwa Leticiah Msole, Mheshimiwa Felix Olombe, Mheshimiwa Bernard Mongo, Mheshimiwa Laurent Marwa na Mheshimiwa Edson Bope. Asante sana! Inapendeza sana mkikaa pamoja namna hiyo. *(Makofi)*

Tunao pia vijana wetu wa *TAYOA* ambao tumekuwa nao tangu mwanzo wakiendelea kujifunza masuala ya demokrasia. Naomba wasimame! Wale pale! Karibuni sana! Natumaini mmejifunza mengi kutokana na kwanza kuingia Ukumbini, lakini pia kukutana na Wabunge nje ya Ukumbi huu. Asante sana, tunawatakia mema katika maisha yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na mkutano wa Tume ya Huduma za Bunge mara baada ya Bunge kuahirishwa. La pili, nimepata vijikaratasi hapa vikiulizia kama leo tutaimba Wimbo wa Taifa kwa mujibu wa Kanuni mpya. Nilitangaza kwamba Kanuni Mpya zitaanza kutumika katika Mkutano wa Kumi, natoa nafasi pia kwa Katibu wa Bunge kuuandaa ule muziki. Hatutaimba tu hivi, kwa sababu baadhi ya sauti humu nazifahamu, haina budi tuongozwe na muziki mahususi wa ala halafu sisi tutafuatiliza! *(Kicheko)*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli tulizokuwa tumezipanga kufanyiwa kazi na Mkutano wa Tisa, zimekwishafanyiwa kazi. Sasa kinachofuata ni Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**SPIKA:** Mtoa Hoja hiyo ni Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu! *(Makofi)*

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kule Kizota Rais alitoa hotuba ya saa 3. Napenda kuwahakikishieni kwamba ya kwangu haitachukua saa 3.

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha Mkutano wa Tisa wa Bunge lako Tukufu ambao ulianza tarehe 30 Oktoba, 2007. Katika Mkutano huu, jumla ya maswali 198 ya msingi na mengine ya nyongeza yalijibiwa na Serikali. Aidha, katika Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili Miswada tisa na kuridhia Maazimio sita.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutumia nafasi hii kuwakumbuka wote waliopoteza maisha yao katika kipindi hiki tangu kuahirishwa kwa Mkutano wa Nane wa Bunge. Hivi karibuni tumempoteza aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia. Hayati Salome Mbatia alikuwa kiongozi mwaminifu, mchapa kazi, anayejituma, shupavu na mpenda watu. Wakati wa mazishi yake, Wahubiri walifananisha kifo chake na mshumaa uliozimika ghafla. Ni dhahiri kwamba tumempoteza kiongozi aliyekuwa mahiri na makini katika kutekeleza majukumu yake. Tunamwombea Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Vilevile, tumempoteza Ndugu Twaha Ngosso, Kada na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wa Wilaya ya Urambo aliyefariki kwenye ajali iliyomhusisha Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pia wamepoteza ndugu, jamaa, marafiki na wapendwa wao. Wengine wamepata maradhi na ajali mbaya ambazo zimewasababishia maumivu hata kupata ulemavu. Nawapa pole sana Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu kwa ajali walizopata. Vilevile nampa pole Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambaye amefanyiwa upasuaji nchini India. Tunawaombea waweze kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa. Aidha, nawapa pole wote waliopata msiba wa

kufiwa na ndugu, jamaa, marafiki wapendwa wao katika kipindi hiki. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu Mahala Pema Peponi. Amin.

Vifo vingi na majeruhi vimetokana na ajali mbaya za barabarani. Natoa wito kwa madereva kuendesha kwa uangalifu huku wakitambua kuwa wamebeba roho za watu. Kwetu sote na hasa vyombo vya dola ni kuhakikisha madereva wanafuata sheria za barabarani. Vilevile, kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya usafiri vinakidhi ubora unaohitajika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kufanya Mkutano wake Mkuu wa Nane kwa mafanikio makubwa. Chama cha Mapinduzi kimeendelea kuwa darasa la demokrasia ndani ya vyama vya siasa nchini. Napenda kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. Kwa namna ya pekee, nampongeza kwa hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa CCM. Hotuba hiyo iliyosheheni masuala makubwa yanayohusiana na mustakabali wa nchi yetu kiuchumi, kisiasa na kijamii imesawazisha hali ya kisiasa nchini. Tuna imani kubwa kuwa chini ya uongozi wake, CCM itaendelea kuwa imara na nchi yetu kuendelea kuwa kisiwa cha amani na watu wenye mshikamano.

Vilevile nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Tanzania Zanzibar na Mheshimiwa Pius Msekwa kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Tanzania Bara. Nampongeza pia Mheshimiwa John Samwel Malecela aliyepumzika Umakamu wa Mwenyekiti wa CCM. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Pia nawapongeza wale wote waliochaguliwa na Mkutano Mkuu kujiunga na Halmashauri Kuu ya Taifa. Nawapongeza vilevile wale wote waliochaguliwa na kuteuliwa kuingia katika Kamati Kuu na Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, Katibu Mkuu wa CCM. Hongereni Sana! Nitakuwa sina fadhila kama sitawashukuru Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu. Asanteni Sana! Nakupongeza wewe Spika na wenzako kwa kusimamia vizuri uchaguzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu wa Tisa wa Bunge lako Tukufu umepitisha Miswada ifuatayo:

(i) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007.

(ii) Muswada wa Sheria wa Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2007.

(iii) Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Mionzi wa Mwaka 2007.

(iv) Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Maabara za Afya wa Mwaka 2007.

(v) Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007.

(vi) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Usajili wa Wahandisi wa Mwaka 2007.

(vii) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007.

(viii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho katika Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007.

Katika mkutano huu, Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI wa Mwaka 2007 ulisomwa kwa mara ya kwanza. Nia ya Muswada huu ni pamoja na kuchukua hatua kali kwa wale wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati za Miundombinu, Uwekezaji na Biashara, Maendeleo ya Jamii na Taarifa ya Benki ya Rasilimali. Wakati wa majadiliano hayo, Bunge lako Tukufu lilikubali kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza Mkataba wa Umeme wa Dharura wa Kampuni ya *Richmond*. *(Makofi)*

Aidha, Mheshimiwa Rais ameunda Kamati ya Kuangalia Upya Mikataba ya Uchimbaji wa Madini nchini. Serikali inaahidi kutoa ushirikiano wa karibu kwa Kamati zilizoteuliwa ili ziweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake. *(Makofi)*

Mwisho, Bunge lako Tukufu liliridhia Azimio la mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Azimio la Kuanzisha Hifadhi Mpya ya Taifa Mkomazi, Azimio la Kupanuliwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji. Vilevile Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Bunge Kuridhia Waziri wa Fedha kufuta na kusamehe madai na hasara zitokanazo na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, malipo batili, madai ya kodi pamoja na maduhuli yasiyokusanyika kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006. Aidha, Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya *NEPAD* kuhusu Mwongozo wa Sera na Udhibiti wa Ujenzi wa Mkongo wa TEKNOHAMA wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini liliridhiwa. Michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadiliano ya taarifa na maazimio haya inatupa changamoto ya kuboresha huduma kwa wananchi na wajibu wa Serikali katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa nitasema kidogo juu ya uimarishaji wa Masoko ya Mazao ya Wakulima. Moja ya changamoto ambazo Serikali inakabiliana nazo ni lile linalohusu masoko ya mazao ya wakulima. Wakulima wamekuwa wakilalamika kuhusu

kupunjwa na mawakala wa kati na hata walanguzi na hivyo kutonufaika na mazao yao. Moja ya majukumu ya Serikali ni kuweka mazingira yatakayowawezesha wakulima kunufaika kwa kiwango kikubwa na jasho lao. Hatua ambazo Serikali imezichukua ni kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Huu ni utaratibu ambao umeanzishwa chini ya Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo nchini. Mfumo huu unawasaidia wakulima kuondoa walanguzi wa kati katika soko. Aidha, unawawezesha wakulima kutumia mazao yao kama dhamana kupata mikopo kutoka benki wakati wakisubiri bei za mazao yao ziwe nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani unaweza kutumika katika mazao yote ya biashara na chakula nchini ambayo hayaharibiki haraka. Hata hivyo, matumizi ya mfumo huu hutofautiana kati ya mazao ya chakula na yale ya biashara kutokana na mabadiliko ya bei na mfumo wa ununuzi wa mazao husika. Kwa upande wa mazao ya chakula kama vile mahindi na mpunga uzoefu umeonyesha kuwa yamekuwa na tofauti kubwa ya bei kati ya kipindi cha mavuno na miezi michache baada ya mavuno. Wakulima wengi wa mazao haya ya chakula wanafahamu tofauti hii kubwa ya bei. Chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao inatambulika kuwa mazao yakiwa ghalani bado ni mali ya mkulima na ndiye anayehusika na utafutaji wa soko. Bei atakayopata hata ikizidi ile aliyoingia nayo mkataba na Benki faida yote inabaki kwa mkulima. Hivyo kupitia mpango huu wakulima wengi wa mahindi na mpunga katika maeneo mbalimbali ambapo Programu inatekelezwa wameweza kupata bei nzuri miezi michache baada ya mavuno.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mafanikio hayo, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani umeonyesha kuwa na manufaa makubwa kwa mkulima. Mfumo huo unamwezesha mkulima kuhimili ushindani uliopo sokoni. Kwa mfano, katika msimu wa mwaka 2006/2007, jumla ya wakulima 582 kutoka wilaya za Mbarali, Hanang, Babati, Njombe, Mbeya Vijijini na Sumbawanga wameweza kufaidika kwa kuuza jumla ya tani 5,849 (mpunga tani 3,714 na mahindi tani 2,135) kupitia mfumo huu na kupata ongezeko la mapato la shilingi bilioni 1.1. Ongezeko hili limetokana na bei za mazao kama ifuatavyo:

(a) Kwa upande wa mpunga ambapo walihifadhi tani 3,714: kipindi cha mavuno bei ilikuwa shilingi 180 kwa kilo. Baada ya miezi minne (4) bei ilipanda hadi shilingi 430 kwa kilo. Hili ni ongezeko la shilingi 250 kwa kilo, sawa na asilimia 155.5.

(b) Kwa upande wa mahindi ambapo walihifadhi tani 2,135: bei ya kipindi cha mavuno ilikuwa shilingi 90 kwa kilo. Baada ya miezi minne (4) bei ilipanda hadi shilingi 170 kwa kilo. Hili ni ongezeko la shilingi 80 kwa kilo, sawa na asilimia 88.9.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya biashara, hali ni tofauti kidogo ambapo mabadiliko ya bei yanategemea zaidi soko la dunia. Kwa maana hiyo, mkulima hawezi kushawishika kuhifadhi mazao yake ili apate bei nzuri. Katika hali hiyo, matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwa mazao ya biashara unaweza kumsaidia mkulima kama tu lengo litakuwa ni kumwezesha kupitia chama chake cha

ushirika, kuongeza thamani ya mazao yake kwa kusindika au kubangua mazao hayo au kutafuta soko.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwa mazao ya biashara, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(i) Makubalianao ya matumizi ya Stakabadhi za Mazao Ghalani yawe kati ya Chama cha Ushirika (kwa niaba ya wakulima), mtunza ghala na benki. Kwa mpangilio huo, benki itatoa mkopo kwa Chama cha Ushirika kwa dhamana ya mazao yaliyowekwa na wakulima;

(ii) Mkulima lazima alipwe bei halisi ya soko wakati analeta mazao yake ghalani na isiwe ni mkopo;

(iii) Mkulima apewe ahadi ya malipo ya pili mara baada ya mazao kuuzwa kulingana na kiasi cha mazao ambayo mkulima aliuza kwenye Chama cha Ushirika na bei halisi ya soko; na

(iv) Kadri inavyowezekana Chama cha Ushirika kisindike au kibangue mazao hayo ili kuyaongezea thamani kabla ya kuyauza kwa wanunuzi wa ndani na nje. Sehemu ya faida itakayopatikana igawanywe kama malipo ya pili kwa wakulima wote waliouza mazao yao kupitia kwenye chama chao cha ushirika. Hii itawafanya wakulima waone faida ya ongezeko la thamani kwa mazao yao. Malipo haya ya pili yataamuliwa na wanachama wote kwenye mkutano mkuu. Hii ni moja ya dhana za ushirikishwaji wa wananchi katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani yanatokana kwa kiasi kikubwa na ushirikishwaji na uwezeshwaji wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao. Natoa wito kwa viongozi na watendaji wote kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono utaratibu huu kama njia bora ya kuwaondolea wananchi kero ya kunyonywa na walanguzi ili nao wapate kunufaika na jasho lao.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lina umuhimu mkubwa katika kuwawezesha wananchi kupambana na umaskini ni lile la kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba benki, kukopa kwa busara na kurejesha mikopo kwa wakati. Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kutambua umuhimu huo imehimiza Serikali kuweka mazingira mazuri ya kujenga tabia ya kujiwekea akiba miongoni mwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo. Ni dhahiri kuwa tukijenga utamaduni huu utatuwezesha kuanzisha miradi endelevu ya kiuchumi ya wananchi itakayoharakisha kuondoa umaskini nchini. Miongoni mwa manufaa na faida za kuweka akiba ni pamoja na:-

(i) Kuweka akiba kunawezesha wananchi kufahamu mtiririko wa mapato yao na jinsi ya kupanga matumizi endelevu na yenye manufaa ya kuwaletea maendeleo;

(ii) Kujiwekea akiba kunasaidia kupata mikopo kutoka benki na kuanzisha shughuli au miradi mbalimbali ya maendeleo;

(iii) Kuweka akiba benki kunawawezesha wananchi kuepuka athari za kupotea kwa fedha zao kwa njia mbalimbali; na

(iv) Bila kuweka akiba ni vigumu kuwekeza. Wataalamu wa uchumi wanatuambia kuwa upo uwiano mkubwa sana baina ya kiwango cha kuweka akiba ikilinganishwa na kiwango cha uwekezaji wa mitaji kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuweka akiba benki na kwenye masoko ya mitaji ndio njia bora na ya kisasa ya kutunza fedha na kuzitumia kwa busara. Huu ndio msingi wa kuwa na wajasiriamali makini. Wale wote wanaoweka akiba, wasiokula mitaji, wanaowekeza faida, wanahitimu na kuwa wafanyabiashara wazuri na siyo wachuuzi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa Nchi Zilizoendelea ziliweza kuwekeza mitaji na kupata maendeleo makubwa kutokana na wananchi wake na nchi kwa ujumla kuwa na utamaduni wa kuweka akiba. Hivi sasa nchi ya China ndiyo inayoongoza duniani kwa kuwa na kiwango kikubwa cha kuweka akiba cha asilimia 50 ya Pato la Taifa. Nchi nyingine za Bara la Asia nazo zina viwango vya kuridhisha vya kuweka akiba ya takriban asilimia 30 ya Pato la Taifa.

Kwa upande wetu, kiwango cha kuweka akiba nchini cha asilimia 12 ya Pato la Taifa bado ni kidogo sana ingawa kiwango hiki hakitofautiani sana na vile vya jirani zetu. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, viwango ni asilimia 11.2 kwa nchi ya Uganda na asilimia 14.5 kwa nchi ya Kenya. Ni dhahiri kuwa viwango hivi bado ni vidogo. Wataalamu wanashauri kuwa kiwango cha chini cha uwekaji akiba kinachoweza kuondoa umaskini na kuharakisha ukuaji wa uchumi ni asilimia 30 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Serikali imechukua hatua madhubuti za kujenga jeshi imara la wajasiriamali nchini. Hali hii imeanza kuwajengea wananchi wetu utamaduni wa kujiwekea akiba na kukopa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha ushirika hasa ule wa kuweka na kukopa *(SACCOS/SACAS),* pamoja na kutekeleza sera na programu na miradi mbalimbali. Lengo la kuchukua hatua hizi ni kuongeza kasi ya kupiga vita umaskini na kuwainua kiuchumi wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, chini ya programu na miradi hiyo, jitihada zinazofanywa na Serikali zimeonyesha matunda ya kuridhisha. Nitataja baadhi ya mafanikio. Mfano, kupitia mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, hadi Septemba 2007, jumla ya wajasiriamali 36,512 wamekopeshwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 29 iliyotolewa na Benki za *CRDB* na *NMB*. Ili kuendeleza jitihada hizi Serikali imeamua kuingia katika awamu ya pili ya utoaji mikopo ya ujasiriamali ambapo mikopo itatolewa kupitia mabenki na asasi za huduma za fedha zenye mitaji midogo midogo zinazokopesha wajasiriamali vijijini. Asasi hizi zina ujuzi, uzoefu na mtandao mkubwa unaoweza kuwafikia wananchi wengi vijijini. Serikali ina matumaini kuwa kupitia mfumo huu, wananchi wengi watapata fursa ya kupata mikopo ya uwezeshaji hasa katika maeneo au wilaya ambazo huduma za Benki za *NMB* na *CRDB* hazijafika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Novemba, 2007, Serikali ilikutana na mabenki na asasi ndogo ndogo zinazotoa mikopo vijijini. Asasi hizo ziliafiki kuanza kutoa mikopo hiyo ndani ya kipindi cha mwezi mmoja. Hivi sasa Benki Kuu ya Tanzania inakamilisha makubaliano na kuwekeana mikataba na asasi hizo ili utoaji mikopo uanze mapema Desemba, 2007. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itatoa kipaumbele na kuweka utaratibu wa kuwezesha mikopo ya ujasiriamali kutolewa kwa wilaya ambazo bado hazijafikiwa katika mfumo wa kwanza. Asasi husika zitapangiwa maeneo kwa kuzingatia lengo hilo. Napenda kutumia fursa hii kutaja benki na asasi ambazo zimeonyesha utayari wa kushiriki kwenye mpango huu ambazo ni:

(i) Benki ya Posta ambayo ina matawi 23 katika mikoa 16 nchini ambayo ni Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Kagera, Manyara, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Pia Benki hii ina tawi moja Zanzibar;

(ii) Muungano wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo nchini *(SCCULT)* ambao una matawi katika mikoa yote;

(iii) DUNDULIZA ambao wana matawi katika mikoa ya Ruvuma, Mara, Mwanza na Dar es Salaam;

(iv) Akiba *Commercial Bank* ambayo ina matawi 7 katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha;

(v) *PRIDE* ambayo ina matawi katika mikoa yote nchini; na

(vi) *Presidential Trust Fund* ambao wana matawi 7 katika wilaya za Kinondoni, Ilala, Morogoro Mjini, Kibaha, Chalinze, Turiani na Makambako.

Asasi nyingine ambazo zipo tayari ni:

(a) Benki ya Wananchi Mbinga (Ruvuma);

(b) Uchumi *Commercial Bank* (Kilimanjaro);

(c) Benki ya Wananchi Mufindi (Iringa);

(d) Benki ya Wananchi Mwanga (Kilimanjaro);

(e) Kagera *Farmers Cooperative Bank* (Kagera);

(f) Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (Kilimanjaro); na

(g) Azania *Commercial Bank* (Dar es Salaam na Mwanza).

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa na yanaendelea kutolewa kwa wananchi ili watambue umuhimu wa kuweka akiba, kukopa kwa busara na kulipa kwa wakati. Pia mafunzo katika kila Halmashauri yametolewa kwa Wataalamu wa Halmashauri na Benki husika ili kuwawezesha wajasiriamali kuibua miradi mizuri na endelevu inayokopesheka. Utaratibu huu ukijengeka vizuri dhana ya kujiwekea akiba itaimarika.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuhamasisha vyombo vya fedha ili vitoe mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wakiwemo wanawake na vijana. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha. Utekelezaji wa mpango huu unaendelea vizuri kupitia mpango wa kuanzisha na kusambaza huduma za benki zinazotoa mitaji midogo midogo vijijini (*Microfinance Institutions (MFIs*). Kutokana na jitihada za kuwahamasisha wananchi kuanzisha vikundi mbalimbali vya ushirika, hadi Septemba, 2007, kulikuwa na Vyama vya Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa *(SACCOS)* vipatavyo 3,469 ikilinganishwa na vyama 1,635 vilivyokuwepo mwezi Juni, 2005. Hili ni ongezeko la vyama 1,834, sawa na asilimia 112.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wazuri wanafahamu kuwa ukipata faida huna budi kutenga faida yako katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza kwa ajili ya kuwekeza ili kuendeleza biashara na sehemu nyingine kwa ajili ya kuweka akiba. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge watakaporejea katika majimbo yao kuwahamasisha wananchi kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba kwa maendeleo yao. *SACCOS* tulizozianzisha vijijini nyingi zinahitaji kuimarishwa ili ziweze kutoa huduma bora pamoja na kuhamasisha wananchi kujiwekea akiba. Kuweka akiba ni fursa ya pekee ya kujiletea maendeleo. Bila kuweka akiba ni wazi huwezi kupata mtaji kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Tanzania bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji mdogo wa mbolea, mbegu bora, zana za kisasa, matumizi ya teknolojia duni, uhaba wa miundombinu, uhaba wa masoko na kutegemea kilimo cha mvua. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizi na baadhi ya mafanikio yamepatikana hasa katika ongezeko la uzalishaji na tija katika baadhi ya maeneo. Pamoja na mafanikio hayo, uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ungekuwa mkubwa kama Watanzania tungekuwa tunatumia teknolojia sahihi, mbolea, mbegu bora, huduma za ugani na zana za kisasa za kilimo katika kuzalisha mazao mbalimbali hapa nchini. Kwa mfano, takwimu za mwaka 2006/2007 zinaonyesha kuwa:

(i) Tulilima hekta milioni 2.6 za mahindi na kuvuna tani milioni 3.66. Huu ni wastani wa tani 1.4 kwa hekta. Kama tungetumia teknolojia sahihi, zana za kisasa, mbolea na mbegu bora za kilimo tungeweza kuzalisha wastani wa tani 5 kwa hekta na hivyo kupata mahindi tani milioni 13.4;

(ii) Tulilima mpunga hekta 558,100 na kuvuna tani 917,200 sawa na wastani wa tani 1.6 kwa hekta. Kwa kutumia teknolojia sahihi, zana za kisasa, mbolea na mbegu bora za kilimo tungeweza kuvuna wastani wa tani 4.0 za mpunga na kupata tani milioni 2.2 za mpunga;

(iii) Tulilima mtama hekta 830,600 na kuvuna tani 915,745, sawa na wastani wa tani 1.1 kwa hekta. Tungeweza kuvuna wastani wa tani 3 kwa hekta na hivyo kupata tani milioni 2.49 za mtama kama teknolojia sahihi, zana na mbegu bora za kilimo zingetumika;

(iv) Kwa zao la chai, tulilima hekta 22,714 na kuzalisha tani 31,348 za chai, sawa na wastani wa tani 1.38 kwa hekta. Kama tungetumia teknolojia sahihi na zana bora za kilimo tungeweza kupata wastani wa tani 2 kwa hekta na kuvuna tani 45,428; na

(v) Kwa zao la kahawa tulilima hekta 247,600 na kuvuna tani 52,000, sawa na tani 0.21 kwa hekta. Kwa kutumia teknolojia sahihi na zana bora za kilimo tungevuna wastani wa tani 2 kwa hekta na kupata tani 495,200 za kahawa.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji huu ni mdogo hasa ukilinganisha na nchi jirani kama ifuatavyo:

(i) Malawi wanazalisha wastani wa tani 2.41 za chai kwa hekta, sukari wanazalisha tani 16.13 kwa hekta. Wakati Tanzania inazalisha tani 1.38 za chai na tani 4.14 za sukari kwa hekta.

(ii) Kenya nao wanazalisha wastani wa tani 2.20 za chai kwa hekta.

(iii) Uganda wanazalisha kahawa wastani wa kilo 520 kwa hekta wakati Tanzania inazalisha wastani wa kilo 210.

Ni dhahiri kwamba matatizo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo (mbolea na mbegu bora), upungufu wa huduma za ugani pamoja na kutumia zana duni za kilimo yamechangia sana katika kuwa na uzalishaji mdogo. Ndio maana wenzetu wa nchi jirani wanatuzidi kwa uzalishaji na tija. Tunahitaji kubadili mwelekeo huu vinginevyo kuna uwezekano wa kuendelea kuwa na soko la mazao ya wenzetu.

Mheshimiwa Spika, wakati anafungua Mkutano Mkuu wa Nane wa CCM tarehe 3 Novemba, 2007, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alituasa kwa kusema yafuatayo:

> *"Kilimo huchangia asilimia 40 ya pato la Taifa na asilimia 30 ya mapato ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, kuinua uchumi wa nchi yetu na kuinua kipato cha Watanzania walio wengi na kuleta maisha bora, hakuwezi kufanikiwa kama tutaendelea kubaki nyuma kwenye kilimo. Vilevile Ilani inatuelekeza kwamba kuleta mapinduzi katika kilimo ndiyo changamoto kubwa katika mchakato wa kujenga uchumi".*

Changamoto iliyopo kwa wadau wote ni kutekeleza kikamilifu Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ili tuweze kuleta mapinduzi na kuwawezesha Watanzania kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika**,** nizungumze kidogo juu ya zana za kilimo. Eneo moja muhimu katika kilimo ambalo lazima tulipe msukumo mkubwa zaidi ni lile la matumizi ya zana bora. Matumizi ya zana bora za kilimo nchini bado yapo chini ambapo wakulima wengi wanatumia jembe la mkono.

Takwimu zinaonyesha kuwa kuna majembe ya mkono milioni 14, majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 667,203 na matrekta 7,200. Kilimo cha wanyamakazi ni cha muhimu sana kwa nchi ambayo haina idadi kubwa ya matrekta. Mikoa inayoongoza kwa kilimo cha wanyamakazi hadi sasa ni Shinyanga, Manyara, Singida na Rukwa, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Katika Mikoa hiyo, eneo linalolimwa kwa kutumia wanyamakazi ni zaidi ya asilimia 50. Mikoa mingine yenye fursa kubwa ya kutumia wanyamakazi ni Mara, Tabora, Mwanza, Iringa, Dodoma na Arusha. Natoa changamoto kwa Mikoa yote yenye fursa ya kutumia wanyamakazi katika kilimo kuongeza idadi inayotumika sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo letu la Afrika Mashariki, kilimo cha kutumia jembe la mkono Tanzania ni asilimia 70, Uganda asilimia 90, wale wanalima kahawa na migomba hawahitaji sana matrekta, lakini na Kenya asilimia 50. Eneo linalolimwa kwa kutumia wanyamakazi nchini Kenya na Tanzania ni asilimia 20 na asilimia 8 nchini Uganda.

Mheshimiwa Spika, aidha, kilimo cha kutumia matrekta ni asilimia 2 nchini Uganda, asilimia 10 Tanzania na asilimia 30 Kenya. Tukilinganisha na wenzetu wa Afrika ya Kaskazini asilimia 20 inalimwa kwa jembe la mkono, asilimia 20 kwa wanyamakazi na asilimia 60 kwa kutumia matrekta.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, inatuelekeza kubuni mpango kabambe wa kueneza matumizi ya plau za kuvutwa na maksai nchini kote ukiondoa kule ambako mazingira hayaruhusu**.** Katika kutekeleza maelekezo hayo Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kutoa mikopo ya ununuzi wa matrekta mapya**.** Mfuko wa Taifa wa Pembejeo pamoja na udogo wake umeweza kutoa mikopo ya kununua matrekta mapya na kukarabati matrekta chakavu. Kwa kipindi cha miaka mitatu, jumla ya shilingi bilioni 5.11 zimekopeshwa kwa kununua matrekta mapya 160 na shilingi milioni 939.815 zimekopeshwa kwa kukarabati matrekta chakavu ya wakulima.

(ii) Usambazaji wa teknolojia rahisi ya matrekta ya mkono. Teknolojia ya kutumia matrekta ya mkono imewavutia wakulima wengi na kuleta ongezeko la mahitaji kwenye mashamba ya mpunga na hivyo kurahisisha kilimo kwa wakulima wadogo wadogo.

Mwaka 2006/2007, jumla ya matrekta ya mkono 325 yameingizwa nchini ambapo kati ya hayo 51 yamekopeshwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo.

(iii) Kuongeza matumizi ya kilimo cha wanyama kazi. Serikali imekarabati vituo 55 vya wanyama kazi na kuvipatia zana bora za kilimo pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali kwa kutumia mashamba darasa. Zana hizo ni pamoja na plau, majembe ya palizi, majembe ya matuta, jembe la tindo, mashine za kupanda mbegu na mikokoteni.

Mheshimiwa Spika, Changamoto inayotukabili kama Taifa, ni kuandaa mkakati maalumu wa kuhakikisha kuwa zana za kilimo zinapatikana kwa wakati na bei za kuridhisha kwa wakulima. Ni wajibu wa kila Mkoa na Wilaya kuwa na mpango wenye malengo yanayopimika kuelekea kwenye kueneza matumizi ya plau nchini kote. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira yatakayowezesha utengenezaji na upatikanaji wa mikokoteni ya kuvutwa na wanyama na vinu vya kisasa vya kukobolea na kusagia nafaka ili viwafikie wakulima wengi. Hii ni katika kusaidia kuleta mapinduzi ya kilimo, hatuna mpango mbadala kama tunataka kukibadili kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie nafasi ya elimu ya ufundi na mafunzo katika kuongeza ajira**.** Moja ya eneo muhimu lililopata mjadala ndani ya Bunge lako Tukufu kipindi hiki ni lile linalohusu uimarishaji wa elimu ya ufundi nchini. Niliwafurahia sana baadhi ya Wabunge ambao sikujua walikuwa ni mainjinia wakabadilisha *profession* kwenda kuwa wanasheria kwa sababu ya matatizo katika sekta hii. (*Makofi*)

Suala hili lilizungumzwa wakati wa kujadili Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Ufundi cha Arusha kuwa chuo kinachojitegemea kiutendaji. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshiriki kwenye mjadala huo, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imepanua wigo wa soko la ajira. Hata hivyo, soko hili litakuwa ni soko la ushindani mkubwa unaohitaji stadi na ujuzi. Elimu na mafunzo ya ufundi ni muhimu katika kuiwezesha nchi yetu kumudu ushindani katika soko la ajira. Elimu ya ufundi ninayoizungumzia ina maana pana kuhusisha fani mbalimbali. Elimu hii ya ufundi inatoa ujuzi, stadi, uelewa na umahiri wa vitendo na nadharia vinavyomwezesha mhitimu kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe katika fani husika. Elimu hii ni nguzo muhimu katika jitihada za Serikali za kukuza uchumi na kupambana na umasikini.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)*, linathibitisha hoja hii kwa kueleza kuwa, na hapa nanukuu kwa Kiingereza: **"***Technical and vocational education and training is increasingly perceived as the master key to poverty eradication and social cohesion."* wanachosema *UNESCO* ni kwamba elimu na mafunzo ya ufundi ni nguzo muhimu katika vita dhidi ya kuondoa umaskini, kwa kweli wanasema ni ufunguo wa kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika**,** suala la elimu ya ufundi limesisitizwa pia katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Msisitizo umewekwa katika maeneo yafuatayo:-

(1) Kuongeza kasi ya upanuaji mafunzo ya ufundi stadi na kushirikiana na sekta binafsi.

(2) Kuanzisha Vyuo vya *VETA* angalau kimoja kwa kila Wilaya kwa lengo la kuongeza nafasi za masomo ya ufundi staid. Changamoto kubwa tuliyonayo ni kuhimiza mafunzo ya ufundi nchini ili kuwawezesha wananchi wetu kushindana katika soko la ajira ambalo linapanuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya ufundi nchini kwa muda mrefu ilipata msukumo mkubwa uliotokana na dira ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere juu ya elimu ya kujitegemea. Elimu hii ililenga kuwa na wasomi wajuzi ambao wataweza kukabiliana na mazingira ya kazi, kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tofauti na elimu inayotolewa na Vyuo Vikuu, elimu itolewayo katika vyuo vya elimu ya ufundi nchini inalenga kuwapa wahitimu umahiri wa utendaji kazi, stadi za kazi na maarifa katika maeneo yao ya taaluma pamoja na ufumbuzi kama alivyotuambia Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Spika, taaluma hizo ni kama vile uandishi wa habari, usafirishaji, madini, kilimo, uvivu. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI** : Uvuvi!

**WAZIRI MKUU**: Sijawahi kuvua ndiyo maana sijui maana ya uvuvi. Uvuvi, Uganga, Hoteli, Ubaharia na kadhalika. Uzoefu umeonyesha kuwa elimu ya ufundi huwawezesha wahitimu kufanya kazi katika taaluma zao bila ulazima wa kuwepo mafunzo ya awali kazini. Pia elimu hii inawapa umahiri na ubunifu wa kufanya kazi kwa vitendo kuzingatia mahitaji ya soko. Hali hii imekuwa kichocheo cha wahitimu kuajiriwa mapema au kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wapo wanafunzi zaidi ya 152,000 wa fani mbalimbali wanaochukua mafunzo ya muda mrefu katika vyuo vyetu vinavyotoa elimu ya ufundi stadi na ufundi wa kati nchini. Kati yao 110,000 wapo katika vyuo vya ufundi stadi na 25,000 katika vyuo vya elimu ya ufundi vya kati. Aidha, kuna wanafunzi 17,000 wanaosomea fani mbalimbali za ufundi katika vyuo vya elimu ya juu vya ufundi. Jumla ya wanafunzi wanaochukua mafunzo ya ufundi ni asilimia 25 ya wanafunzi wote wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu nchini. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na uwezo wa vyuo hivi kudahili.

Kwa mfano, vyuo 203 vilivyosajiliwa na kutambuliwa na Baraza la Vyuo vya Ufundi (*NACTE*), vinadahili kiasi cha wastani wa asilimia 60 ya uwezo wa vyuo hivyo. Hii ina maana kuwa asilimia 40 ya uwezo wa vyuo hivyo haitumiki. Miongoni mwa sababu za hali hiyo ni pamoja na:-

(1) Kukosekana kwa mikopo kwa wanafunzi wanaosomea masomo ya cheti cha ufundi;

(2) Ukosefu wa tuzo endelevu katika elimu ya ufundi hivyo mwanafunzi anapotaka kwenda Chuo Kikuu kusomea shahada analazimika kuomba sawa na mwanafunzi wa kidato cha sita; na

(3) Mitaala ya vyuo vya ufundi haijaweza kuboreshwa ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira hivyo kuwafanya wahitimu kutoweza kushindana katika soko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Vyuo vya *VETA* changamoto bado ni kubwa, hadi sasa Wilaya 78 tu ndizo zenye Vyuo vya *VETA* vya Serikali. Aidha, katika mwaka 2007/2008 Serikali inatarajia kujenga vyuo vingine vitano katika maeneo ya Njiro – Arusha, Lindi, Kipawa – Ilala, Babati na Kibaha.

Nahimiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikishirikiana na viongozi wa Wilaya na Wananchi kuongeza nguvu katika uanzishaji wa Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya uchaguzi.

Katika nchi nyingi zinazoendelea na zilizoendelea zimeweka na zinaendelea kuweka msisitizo katika mafunzo ya elimu ya stadi na ujuzi mbalimbali. Kwa mfano, takwimu za mwaka 2006 zinaonyesha kuwa uwiano wa mwanafunzi wa elimu ya ufundi kwa idadi ya watu kwa Tanzania ilikuwa mwanafunzi mmoja kwa watu 1,618**,** Ghana mwanafunzi mmoja kwa watu 1,304**,** Zimbabwe mwanafunzi mmoja kwa watu 248**,** Korea Kusini mwanafunzi mmoja kwa watu 54 na Canada mwanafunzi mmoja kwa watu 9. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba sisi bado tuko nyuma sana katika kujenga uwezo katika elimu ya ufundi.

Tunahitaji kuweka juhudi zaidi kama tunataka kupata maendeleo ya haraka. Aidha, nchi nyingi za Bara la Asia, kama vile Malaysia, Singapore na Thailand zimepata maendeleo ya haraka kwa kuwekeza sana katika sayansi, teknolojia na ufundi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuna ushahidi thabiti kuwa nchi ambazo zina maendeleo makubwa duniani ni zile zilizowekeza katika elimu ya ufundi na ile ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Nchi kama vile Marekani, Canada, Ujerumani, Uingereza, Australia, Japan, Korea na sasa India na China zimefikia maendeleo makubwa kutokana na kuwekeza katika elimu ya ufundi. Kwa mfano, kati ya mwaka 1990 na 2000, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi nchini India iliongezeka kwa asilimia 92.

Korea ya Kusini, inapeleka wanafunzi zaidi ya 50,000 kwa mwaka huko Marekani kusoma katika vyuo vya ufundi. Maendeleo yaliyopo katika nchi hizo hayahitaji maelezo ya ziada. Hayo ni matunda ya kuwekeza katika elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kuelewa umuhimu wa vyuo vya ufundi vya juu katika kujenga kada ya wataalamu wenye ujuzi na stadi maalumu, Serikali imesitisha utaratibu wa kuvibadili vyuo hivyo kuwa vyuo vikuu. Serikali imefanya hivyo kwa kutambua

kuwa yapo mahitaji makubwa katika soko la ajira kwa wataalamu wanaohitimu kutoka katika vyuo hivyo. Vyuo hivyo vilianzishwa kukidhi matakwa maalumu ya wataalamu wa sekta husika, na mahitaji ya aina hiyo bado yapo.

Kama ilivyo katika nchi nyingine duniani, vyuo vya elimu hiyo vinapaswa kuendelea kutoa mafunzo yanayoendana na madhumuni ya uasisi wake (*purpose of establishment*) bila kubadili hadhi yake. Vyuo hivi vinaweza kutoa tuzo endelevu hadi ngazi ya shahada bila kuwa vyuo vikuu. Napenda kutaja vyuo vya aina hii ambavyo vipo nchi nyingine, ambavyo ni: *Massachuset Institute of Technology* - USA; *Korea Institute of Technology* - South Korea; *Kigali Institute of Technology* - Rwanda; *California Institute of Technology* - USA; na *Indian Institute of Technology* - India.

Hapa nchini tunavyo vyuo vyenye mwelekeo huo kwa fani maalumu, kwa mfano, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Chuo cha Usimamizi wa Fedha. Changamoto iliyo mbele yetu ni kwa wakufunzi kuboresha mitaala ili iendane na wakati. Mitaala hiyo ilenge katika kutoa elimu bora inayowapa wahitimu uwezo wa kushindana katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika**,** ili tuweze kukabiliana na changamoto za utandawazi na kuwawezesha Watanzania wengi kushindana katika soko la ajira la ndani na nje, lazima kuhimiza elimu ya ufundi na teknolojia ya habari na mawasiliano *(TEKNOHAMA).* Hii itatuwezesha kuongeza tija katika uzalishaji, kupiga hatua katika maendeleo ya viwanda na kuharakisha maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini.

Aidha, hii ndiyo njia ya kuongeza kasi ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Suala hili la nafasi ya TEKNOHAMA katika maendeleo ya nchi yetu nitalizungumzia kwa kirefu katika hotuba nyingine. Changamoto iliyo mbele yetu ni kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi na mashirika ya dini kwa lengo la kuimarisha vyuo vilivyopo na kuanzisha vyuo vipya. Aidha, changamoto nyingine ni kuhakikisha kuwa tunao Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi nchini ambao utatuongoza katika kuimarisha elimu hii. Lengo ni kukidhi matarajio ya soko la ndani na lile la Afrika Mashariki na hivyo kutuwezesha kumudu ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika**,** suala langu la mwisho katika hoja yangu leo ni lile tulilolisukuma sana tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani la upanuzi wa elimu ya sekondari. Katika mwaka 2007, jumla ya wanafunzi 774,383 wamefanya mtihani wa darasa la saba. Kwa kiwango cha kufaulu cha asilimia 80 inatarajiwa kuwa wanafunzi wapatao 619,506 watafaulu na hivyo kuhitaji jumla ya vyumba 15,487 vya madarasa.

Mheshimiwa Spika, nimepata taarifa kuwa Mikoa mingi imejipanga vizuri kutekeleza zoezi la kuwapeleka sekondari asilimia kubwa ya wanafunzi watakaofaulu. Kila Mkoa umeweka mikakati na kubuni mbinu mbalimbali za kutekeleza zoezi hili. Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya, watendaji wote

na wananchi kwa jitihada zinazoendelea za kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaofaulu wanajiunga na elimu ya sekondari, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama tulivyokubaliana mwanzoni mwa mwaka huu, na kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaofaulu wanajiunga na kidato cha kwanza, sitegemei kuwa tutakutana tena ili kukumbushana kuhusu suala hili. Napenda kuwahimiza viongozi katika ngazi zote kuendelea kusimamia kwa karibu zoezi la ujenzi wa madarasa na kuzidi kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuchangia elimu kwa kujenga shule za sekondari. Hata hivyo, ni wajibu wa Wakuu wa Wilaya kote nchini kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa taarifa za mapato na matumizi ya fedha zilizokusanywa na jinsi gani zilivyotumika. Kama nilivyosema hapo awali, bila kuwekeza katika elimu mkakati wetu wa kuondokana na umasikini hautafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nawasihi Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha kuwa wanafunzi zaidi ya asilimia 85 watakaofaulu darasa la saba mwaka huu wanajiunga na kidato cha kwanza mwaka 2008. Inawezekana na mifano halisi ni ile mikoa iliyopeleka wanafunzi sekondari kwa asilimia mia mwaka 2007. Lakini ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza sana mikoa miwili ambayo wakuu wao wa mikoa wanaendelea kuhangaika vizuri sana, Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam, kazi wanayofanya inafaa kuigwa na wengine.

Ongezeko la shule za sekondari limesababisha vilevile ongezeko kubwa la mahitaji ya Walimu. Serikali inatambua tatizo kubwa la walimu hivi sasa na itachukua hatua zote zinazopasa kukabiliana nalo ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu ya sekondari kwa ubora unaohitajiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nchi yetu inazo fursa nyingi za kuweza kujiletea maendeleo. Tunazo fursa za uwekezaji. Tunayo nafasi ya kuwawezesha wananchi wetu kushiriki katika mikakati ya kujitoa katika umaskini, kushiriki kwao ndio maendeleo yao.

Mambo ya msingi ninayoyasisitiza ni haya yafuatayo:-

(i) Tuwahimize wananchi watumie fursa ya Mradi wa Stakabadhi za Mazao Ghalani ili waweze kufaidika na bei nzuri za mazao baada ya kuyahifadhi na hivyo kuwawezesha kupambana na mawakala wa kati wanaowanyonya.

(ii) Tujenge utamaduni wa kujiwekea akiba. Aidha, tuwakumbushe wananchi dhana ya kukopa kwa busara na kurejesha mikopo kwa wakati kwa ajili ya maendeleo yao. Upo msemo usemao, **“***ulimi mtamu utumikao kuomba mkopo sio utumikao mkopo urejeshwapo***”.** Tuhimize utamaduni wa kurejesha mikopo kwa wakati.

(iii) Kilimo bado ndicho mhimili wa maendeleo ya wananchi walio wengi. Tuwakumbushe wananchi kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi, mbolea, mbegu bora na zana za kisasa za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

(iv) Elimu ya ufundi ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Tuelekeze nguvu zetu katika kuimarisha Vyuo vya Ufundi vilivyopo na kuanzisha vipya kwa manufaa ya nchi yetu; na

(v) Tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wote watakaofaulu mtihani wa darasa la saba wanapata nafasi kuingia sekondari. Nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono juhudi zilizoonyeshwa na Mikoa katika kujenga madarasa ya kutosha.

Mheshimiwa Spika**,** napenda kuwashukuru wote waliosaidia katika kufanikisha Mkutano huu. Nikushukuru kwa namna ya pekee wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri, lakini nikupongeze kipekee kwa umahiri wako wa kusimamia Kanuni mpya za Bunge letu, hongera sana. *(Makofi)*

Namshukuru Mwanasheria Mkuu na wataalamu wake kwa kazi nzuri sana waliyofanya katika Bunge hili. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa msaada mkubwa waliotoa wa kuliongoza Bunge hili.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mbalimbali wakati wa kujadili Miswada tuliyoipitisha katika mkutano huu. Namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka na Wasaidizi wake pamoja na wataalamu wote wa Serikali kwa misaada yao ya kitaalamu na ya huduma mbalimbali katika kufanikisha Mkutano wetu. Navipongeza vyombo vya habari kwa kazi nzuri ya kuwafikishia wananchi habari kwa wakati na kwa usahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika**,** katika wiki chache zijazo, tutakuwa tumefika mwisho wa mwaka 2007. Napenda kutumia nafasi hii kumuomba Mwenyezi Mungu atujalie sote tuweze kumaliza mwaka huu salama. Aidha, nawatakia nyote Sikukuu Njema ya *Idd El Haj, Krismas* Njema na Kheri ya Mwaka Mpya! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika**,** baada ya kusema hayo, nawatakia wote safari njema kurudi katika majimbo yenu, naomba msikimbie sana mwende taratibu. Na sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 29 Januari, 2008 saa 3.00 asubuhi, litakapokutana Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa niaba yenu nyote kwa hakika mngependa nimshukuru kwa hotuba hiyo nzuri iliyoonyesha mwelekeo wa maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Kabla sijawahoji kuiamua ninalo tangazo moja ambalo nililiruka. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anawaalika Wabunge wote kwenye sherehe ya

kutunuku wanafunzi 13 wa kitanzania walioshinda shindano la uandishi wa insha la Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, *(SADC)*, lilikuwa shindano la Kanda, vijana wetu 13 wameshinda vizuri. (*Makofi*)

Sherehe hizo zinafanyika leo alasiri katika ukumbi wa chuo cha *VETA*, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tafadhalini saa tisa alasiri kutakuwa na viburudisho na madoido mengine ambayo yanastahili, nadhani ni kitu kizuri kumalizia shughuli za Bunge tulizokaa hapa wiki tatu.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya kuliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 29 Januari, 2008, Saa 3.00 asubuhi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 5.22 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 29 Januari, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*